

IBADA YA KILA SIKU

TOLEO LA 3

Jul-Ago-Sep 2020

# HabariNjema

## KILA SIKU

**BURE**
**HAKIUZWI**
KITABU HIKI CHA IBADA KIMESHALIPIWA NA WASHIRIKA WETU HIVYO NI BURE.

KAMA VILE MAJI YA BARIDI KWA MTU MWENYE KIU, NDIVYO ILIVYO HABARINJEMA ITOKAYO KATIKA NCHI YA MBALI. [MITHALI 25:25]


*Uebert & BeBe*
ANGEL


SPIRIT EMBASSY
TheGoodNewsChurch®
WITH UEBERT & BEVERLY 'BeBe' ANGEL

SPIRIT EMBASSY
TheGoodNewsChurch



## UEBERT & BEBE ANGEL

Wakiwa na miaka mingi ya kufanya huduma ya Mungu, Uebert na Bebe Angel ni mapainia na sauti zinazoongoza kwenye kutangaza habari njema ya neema ya Mungu (Euangelion) pamoja na unabii duniani kote.

Kwa pamoja ni waandishi bora wa vitabu kama Habari Njema, Intimacy, Prayer Banks, Supernatural power of the Believer n.k. Uebert na Bebe Angel ni wazungumzaji wanaotafutwa kwenye mikutano sehemu mbalimbali duniani, ni viongozi wa kidunia. Wanatambulika na kuheshimika kwa maono yao, uvumbuzi na ujasiri wao. Kama waanzilishi wa Kanisa la Good News (Spirit Embassy), na wenye ofisi ya kinabii, wamegusa maisha ya mamilioni ya watu ulimwenguni kupitia mapenzi yao ya kuvuna nafsi na kuleta ufunuo wa habari njema ya neema ya Mungu (Euangelion).



**Warumi 5:1**
**Kwa hiyo, kwa kuwa tumekwisha kuhesabiwa haki kwa imani, tuna amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo,**

Bwana Yesu aliposulibiwa, alikufa kwa ajili ya kila mtu. Dhambi zako zililipiwa ndani ya Kristo. Alilipa adhabu ya mwisho ya kifo (kifo cha kiroho). Hivyo Mungu haitaji ulipie dhambi zako tena. Unapomwamini Yesu, unafanywa upya katika roho yako.

Sasa una uzima na asili ya Mungu. Wewe ni kiumbe kipya, spishi mpya katika Kristo bila ya kale. Wakati Mungu anakuona, anaona yote ambayo Kristo amefanya kwa niaba yako na matakwa ya haki yameridhika.

Katika Kristo, hatusamehewi bila adhabu; tunahesabiwa haki. Hiyo inamaanisha kutangazwa kuwa hauna hatia, huru kwa kila kosa. Haijalishi umetoka wapi au umefanya nini, kama mtoto wa Mungu, unaweza kupata rehema leo. Unaweza kuja kwa ujasiri kwa Baba kwa sababu tuna amani na Mungu sasa, aleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni kiumbe kipya katika Kristo. Siishi tena chini ya hukumu. Nimehesabiwa haki kwa imani katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Waebrania 4:16



**Marko 7:13**
**Kwa njia hiyo ninyi mnabatilisha neno la Mungu kwa taratibu zenu mlizojiwekea. Nanyi mnafanya mambo mengi ya jinsi hiyo.**

Yesu aliwakemea Wayahudi kwakuwa walifanya Neno la Mungu lisifanye kazi kwa ajili ya mila zao. "Mila" hapa ina maana ya njia yako ya maisha, tamaduni yako ya kibinafsi, na mambo unayoamini.

Ikiwa mambo haya hayakubaliani na Neno la Mungu, hufanya Neno lisiwe na maana maishani mwako, na imani yako hufanywa kuwa batili. Umezaliwa na Neno la Mungu, na maisha yako mapya yana asili yake katika Neno.

Unapoachana na yale ambayo Neno la Mungu linasema katika eneo lolote la maisha yako, utateseka katika eneo hilo. Kama samaki, unapomuondoa majini, hufa kwa sababu umemuondoa kwenye chanzo chake cha maisha. Leo haijalishi nini kitakuja, shikamana na Neno, na utarudi na ushuhuda.

## UKIRI WA KINABII

**Neno la Mungu ni taa na chemli kwa miguu yangu. Nimewekwa kwenye kozi ambayo lazima niifuate. Mafanikio ni yangu kwa jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Matendo ya Mitume 20:32



**Warumi 1:17**
**Kwa maana katika Injili haki itokayo kwa Mungu imedhihirishwa, haki ile iliyo kwa njia ya imani hadi imani. Kama ilivyoandikwa: "Mwenye haki ataishi kwa imani."**

Ujumbe wa imani hufundisha kwamba wakati unapohisi dalili katika mwili wako, unaikemea kwa Jina la Yesu. Unaamuru Shetani atoke!

Walakini watoto wengi wa Mungu wafanywa watumwa kwa hisia zao. Uchungu kidogo au maumivu huwafanya wakimbilie vipoza uchungu. Ni kimetokea kwenye maisha ya kimungu ndani yako?

Umezaliwa na Mungu, na maisha Yake ndani yako hukufanya usiweze kubeba ugonjwa, usiyeweza kabisa kuzidiwa. Haleluya! Imani hufanya kazi kila wakati. Itumie kuunda dunia yako na kuunda hali halisi tukufu unayotaka kupitia katika maisha

## UKIRI WA KINABII

**Imani yangu ni hai na inashinda kila wakati! Hali zinalingana na kukiri kwangu kuliojaa imani, natawala, naongoza na kutawala ulimwengu wangu kwa imani yangu kwa jina la Yesu. Amina.**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 24:10, 1 Yohana 5:4-5



**Yakobo 2:26**
**Kama vile ambavyo mwili pasipo roho umekufa, kadhalika nayo imani pasipo matendo imekufa.**

Kuamini kwako na imani yako lazima zifuatane na hatua inayolingana. Haitoshi kuamini tu. Biblia inatuambia kuwa hata mapepo wanaamini kwa kiwango cha kutetemeka, lakini imani bila matendo imekufa. Hii ndio sababu unaposoma injili, wakati wowote Bwana Yesu alipokuwa akiwaponya wagonjwa, kila mara alidai kwamba walifanya wasichoweza kufanya hapo awali. Alimwambia aliyepooza kando ya dimbwi la Bethesda aamke na kutembea.

Alichukua mchanga, akautemea mate, na kutengeneza macho, kisha akamwambia yule kipofu aende akaoshe na akarudi akiona. Haleluya! Imani haishindwi kamwe, lakini unahitaji hatua inayolingana kuachilia imani hiyo! Tembea kwa imani leo, na utashinda kila vita!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaishi na kutembea kwa imani. Mimi ni zaidi ya mshindi, na imani yangu haifanyi kazi kwa maneno yangu tu bali na matendo yangu kwa jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Yakobo 2, Waebrania 11:1-6



**1 Timotheo 4:15**
**Uwe na bidii katika mambo haya, jitolee kwa ajili ya mambo hayo kikamilifu, ili kila mtu aone kuendelea kwako.**

Ni vema kuponywa kuumwa au ugonjwa wowote, lakini vipi kuhusu kutokuwa mgonjwa? Kwa kuwa umezaliwa mara ya pili, unao uzima wa milele, na uzima wa milele hauitaji uponyaji.

Kwa hivyo, haijalishi ni nini kinachoshambulia mwili wako. Ikiwa unachochea uhai wa Mungu katika roho yako, mwili wako wote utakidhika. Haleluya! Kristo ndani yako - Roho Mtakatifu aliye ndani yako — hutoa nguvu!

Neno la Kiebrania lililotafsiriwa kama, "tafakari" katika andiko letu la leo ni, meletáō, pia linamaanisha "kufanya mazoezi." Matokeo yake ni kwamba maendeleo na mafanikio yako hayawezi kukatalika na kuepukika. Leo ikiwa unahisi dalili zozote za ugonjwa mwilini mwako, ni mihemko. Zikomoe na Neno; kataa kukata tamaa!

## UKIRI WA KINABII

**Uzima wa milele unafanya kazi ndani yangu; kila punje ya uhai wangu imejazwa na maisha ya Mungu. Sitakufa bali naishi, aleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8:11



**Marko 11:23**
**Amin, amin nawaambia, mtu ye yote atakayeuambia mlima huu, 'Ng'oka ukatupwe baharini,' wala asione shaka moyoni mwake, bali aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake.**

Bwana Yesu alionesha utawala kamili juu ya hali za maisha wakati wa huduma Yake hapa duniani, pamoja na nguvu za kiasili. Alitufanya tugundue kuwa tunaweza kuongea na kitu chochote, kushawishi kitu chochote, na kuleta mabadiliko kwa maneno yetu.

Haijalishi ni nyakati gani au hali gani umejikuta umo, unaweza kuleta mabadiliko kwa maneno yako! Maneno yako yana uwezo wa kuchoma kila kitu maishani mwako na katika njia yako ambavyo haviendani na mapenzi kamili ya Mungu.

Maneno yako hutawala maisha yako. Usisahau kamwe. Ni jukumu lako leo kujiweka katika maisha ya ushindi kwa kuongea maneno ya ubunifu ya imani.

## UKIRI WA KINABII

**Neno la Mungu limetimia katika fedha zangu, na nimebarikiwa kuwa baraka kwa wengi. Mimi ni wa ajabu, namfanyia Mungu mambo ya ajabu kwa jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 18:20



**Waebrania 8:12**
**Kwa kuwa nitasamehe uovu wao, wala sitazikumbuka dhambi zao tena!"**

Haijalishi nini kimetokea au ni nini umefanya, Mungu anataka ujue kuwa kwa sababu ya kazi ya Mwanae iliyomalizika, Atakuhurumia udhalimu wako, na dhambi zako na vitendo visivyo halali hatavikumbuka tena.

Ndio maana haipaswi kuziwaza dhambi zako. Kiukweli, unapokuwa na mawazo ya dhambi, ibilisi huleta lawama. Na kadiri unavyoipokea na kujihukumu mwenyewe, ndivyo utakavyojikuta huwi na msamaha kwako na hata kwa wengine.

Kadiri unavyozingatia ukweli kwamba unao msamaha wa Baba na haikulaumu kwa sababu ya kazi iliyomalizika ya Yesu, ndivyo kadri dhambi na matokeo yake - magonjwa, chuki, ukosefu na kadhalika – zitakosa sehemu ya kukushikilia. Utajikuta ukitembea kwa kiwango kikubwa cha neema na baraka za Mungu!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni kiumbe kipya katika Kristo, ninayo amani na Mungu. Upendo wa Mungu umemwagika nje kutoka moyoni mwangu, na ninatembea katika utimilifu wa baraka Zake kwa jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8:1



**Yohana 10:10**
**Mwivi huja ili aibe, kuua na kuangamiza. Mimi nimekuja ili wapate uzima kisha wawe nao tele.**

Wakristo wengi hawaelewi hata ni kwa nini Bwana Yesu alikuja na kufa kwa ajili ya ulimwengu wote. Kusulubiwa kwake na kufufuka kwake ilikuwa njia ya kuleta mwisho. Andiko letu la leo linaelezea kusudi la kuja kwake.

Anasema, nilikuja wapate uzima. Ah, aleluya! Sasa wakati anasema "uzima tele" hapa, haisemi kwamba ulikuwa na kiwango fulani cha maisha na kisha akaja kukiongeza, hapana! Hapo ndipo mahali ambapo wengi wanapakosa. Anazungumzia juu ya aina ya maisha ya Mungu. Alikuja ili uwe na asili na maisha ya Mungu ndani yako!

Maisha kama aliyonayo Mungu ndio sababu ambayo mtume Paulo alipoumwa na nyoka mwenye sumu aliweza kutingisha mkono wake bila kufikiri mara mbili. Alikuwa na aina hii ya maisha ikifanya kazi ndani yake ambayo hakuna sumu ingeweza kumuua, hakuna kirusi kingeshinda! Kama umezaliwa mara ya pili, umepokea haya maisha. Anza kutembea katika nuru ya uliye.

## UKIRI WA KINABII

**Nina uzima wa Mungu ndani yangu. Vitu vyote vinafanya kazi kwa faida yangu. Siwezi kushindwa kamwe kwa jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 14:6, Yohana 5:26



**Waefeso 6:17**
**Vaeni chapeo ya wokovu na mchukue upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu.**

Silaha za ushambuliaji wetu sio za ulimwengu huu. Biblia inapozungumza juu ya silaha kamili ya Mungu, utagundua kuwa vitu vingine vyote vilivyotajwa, kutoka ngao ya imani hadi kifuko cha haki, vyote ni kinga.

Lakini tumepewa silaha moja inayodhalilisha, upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu. Ndugu na dada, unaweza kutumia Neno la Mungu kushinda hali yoyote, na litafanya kazi kila mara. Lakini kabla ya kufurahi, angalia neno la Kiyunani lililotafsiriwa kama 'neno' katika andiko letu la leo ni rhema.

Neno rhema ni neno ambalo mtu fulani hupewa, katika hali fulani, kwa wakati maalum. Unaona, unapokumbana na changamoto maishani, na kurudi chumbani kwako ukaanza kusali kwa lugha zingine, aya ya Biblia ijayo ndani ya roho yako wakati unasali ni rhema kwa ajili ya pito hilo. Chukua upanga huo wa Roho na agiza uponyaji wako, ustawi wako kwa jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Bwana ndiye nguvu ya maisha yangu; Sitaogopa ambacho mwanadamu anaweza kunifanyia. Nimewashinda kwa jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 4:16



**Yohana 5:44**
**Ninyi mwawezaje kuamini ikiwa mnapeana utukufu ninyi kwa ninyi, lakini hamna bidii kupata utukufu utokao kwa Mungu?**

Wengi hupitia maisha wakijaribu kuwa kila kitu kwa kila mtu. Na kwa sababu wamejiwekea jukumu lisilowezekana, huwa katika hali mbaya kila wakati. Hauwezi kumpendeza kila mtu wakati wote.

Kipaumbele chako cha kwanza kinapaswa kuwa yaliyo sawa machoni pa Bwana. Hiyo ndio njia pekee ya kujua kama uko kwenye njia sahihi au la. Tafuta heshima itokayo kwa Mungu. Hiyo inamaanisha utafanya kile ambacho ni cha heshima ikiwa kamera zinaendelea au la.

Katika barua yake kwa Wagalatia, mtume Paulo huwaambia, kama ningejaribu kuwapendeza wanadamu, nisingekuwa mtumwa wa Mungu. Sasa, hawaambii kuwa wasizingatie wengine. Anasema kuwa kama utakuwa wa manufaa, inabidi upate vipaumbele vyako sawa. Tafuta heshima itokayo kwa Mungu.

## UKIRI WA KINABII

**Kwa neema ya Mungu, ninahama kutoka ngazi moja kwenda nyingine, na ananiongoza katika njia Zake za ustawi huku nikimheshimu yeye na yote niliyo nayo kwa jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Wagalatia 1:10



**Warumi 4:20**
**Lakini Abrahamu hakusitasita kwa kutokuamini ahadi ya Mungu, bali alitiwa nguvu katika imani yake na kumpa Mungu utukufu,**

Abrahamu alikataa kuinama wakati hali yake ya asili ilivyokuwa kinyume na kile alichoambiwa Mungu. Biblia inasema hakujikwaa kwa ahadi.

Imani ni ushindi wetu; kamwe haiwezi kushindwa. Hii ndo sababu ya wewe kutosita. Usipelekeshwe na kile daktari asemacho au kwa uchumi wa nchi yako. Shikilia alichosema Mungu. Kila hali nyingine inaweza kubadilika.

Kwa imani, ulipokea uzima wa milele na Roho Mtakatifu kuishi ndani yako. Kwa imani, haki ya Mungu iliingizwa kwenye roho yako. Hivyo, endelea na imani, kimsingi na kitulivu, na ukatae kuhamishwa mbali na tumaini la Injili ambayo umesikia.

## UKIRI WA KINABII

**Hofu, magonjwa, umasikini, na kifo havina nafasi ndani yangu, kwa sababu ninaishi kwa imani katika Neno la Mungu, ambayo ni kichocheo changu cha mafanikio kamili, ushindi, ustawi, na afya ya Kiungu.**

**SOMO LA ZIADA**
Wakolosai 1:23



**Waefeso 3:12**
**Ndani yake na kwa njia ya imani katika yeye twaweza kumkaribia Mungu kwa uhuru na kwa ujasiri.**

Mungu hakufanyi usubirie muujiza. Haanzi kufikiri juu ya kukuponya au kutokuponya baada ya wewe kusema amina. Kwa kweli, ni aina hii ya mawazo ambayo hufanya Wakristo wasali sala zisizo za Kimaandiko, wakimwomba Mungu kwa miujiza aliyolipia tayari.

Hii ndio sababu unakuta kwamba mtu anaweza kuja hapa kwa mara ya kwanza na akapokea muujiza ambao umekuwa ukiungojea kwa miaka mitatu iliyopita. Walakini Mungu habagui watu. Ndugu na dada, kuna ujasiri fulani ambao huja katika kujua kilicho chako katika Kristo, kwa kiwango ambacho miujiza uja kwako kirahisi.

Mungu ametupa ujasiri huo huo katika Kristo, na haupaswi kuwa mwombaji juu ya vitu unavyohitaji. Andiko linasema twende kijasiri kwenye kiti cha neema ili tupate rehema wakati wa uhitaji.

## UKIRI WA KINABII

**Nina roho ya ujasiri; hofu haina nafasi ndani yangu. Mdomo wangu umejazwa leo na maneno yaliyojaa imani. Neema yake inanitosha!**

**SOMO LA ZIADA**
Waebrania 4:16



**1 Petro 2:2**
**Kama watoto wachanga, waliozaliwa sasa, yatamanini maziwa ya kiroho yasiyochanganywa na kitu kingine cho chote, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu,**

Unapozaliwa mara ya pili - au tuseme, mzaliwa kutoka juu - unapompokea Bwana Yesu Kristo, Biblia inasema umezaliwa kwa mbegu isiyoweza kuharibika kwa Neno la Mungu.

Kwa hivyo basi, ikiwa umezaliwa na ni bidhaa ya Neno, hiyo inamaanisha kuwa chanzo chako cha maisha ni Neno lile lile. Roho yako iliyolishwa inahitaji Neno hilo kukua na kukomaa katika mambo ya Mungu.

Unawajibika kwa maendeleo yako mwenyewe. Ndio maana mtume Petro anatuamuru kutamani maziwa yasiyotiwa damu, ya dhati ya Neno ili upate kukua.

Kama ulikuwa na kisu au shoka butu, unachotakiwa kugonga mara moja unaweza kuhitaji kugonga mara kumi. Lakini kadri unavyozidi kukua, ndivyo unavyozaa matunda na kuwa fanisi zaidi. Unaposhikilia Neno, hakuna kitakachowezekana. Utarudi na ushuhuda!

## UKIRI WA KINABII

**Maisha na asili ya Mungu vinafanya kazi ndani yangu kwani mimi ni uzao wa Neno. Ninapoita vitu, vinakuwa kwa jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Matendo 20:32



**Wakolosai 2:15**
**Mungu akiisha kuzivua enzi na mamlaka, alizifanya kuwa kitu cha fedheha hadharani kwa kuziburura kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba wa Kristo.**

Yesu aliharibu mamlaka na nguvu! Aliwapunguza mpaka kutokuwa chochote hadi uwezo wao kututawala. Alifanya tamasha la umma la shetani na mapepo wake.

Hawawezi tena kukukandamiza na magonjwa. Nguvu hizo hazina maana! Ni nguvu zilizonyang'anywa mamlaka! Hatujaribu kuwashinda, kubali tu kwa imani yale Yesu aliyofanya. Alichofanya, Alikufanyia! Ushindi wa Kristo ni ushindi wako. Katika familia yako, Kristo tayari ameshinda ushindi. Dai ushindi huo juu ya Shetani katika fedha zako, katika ndoa yako, na afya yako.

Haijalishi ni changamoto gani unayokabili leo; habari njema ni kwamba Kristo tayari ameshinda ushindi. Adui amepunguzwa kutokuwa kitu, na unaweza kukubali ushindi huo kwako mwenyewe. Anza kutumia mamlaka yako katika Kristo na ufurahie utimilifu wa baraka za Mungu leo.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi si chini ya shetani na majeshi yake. Nimejificha ndani ya Kristo na nimeshinda, kwa kuwa Yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yeye aliye ulimwenguni.**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 4:4



**Warumi 10:8**
**Lakini andiko lasemaje? "Lile neno li karibu nawe, li kinywani mwako na moyoni mwako," yaani, ni lile neno la imani tunalolihubiri.**

Unaona, ili Neno la Mungu likufanyie kazi, lazima liwe katika kinywa chako na moyo wako. Unaweza kuamini kitu moyoni mwako, lakini ikiwa hautatoa sauti au kukisema, haitatimia.

Hii ndio sababu andiko linasema, amini moyoni mwako na kukiri (kutangaza, kutangaza) kufanywa wokovu. Kwa kuwa tuna roho ya imani, tunapaswa kusema vitu tunavyoamini. Kamwe Usiongelee kufeli. Sijui kuhusu wewe, lakini mimi siamini kuhusu kufeli. Siamini kushindwa, hivyo siongelei kushindwa. Ninaamini katika habari njema ya ushindi wetu katika Kristo, aleluya!

Anza kuongelea leo yale ambayo Mungu ameahidi kwenye afya yako. Tangaza mapenzi yake juu ya ndoa yako na fedha. Ushindi ni wako katika Kristo, na unaweza kuushughulikia leo. Fungua tu mdomo wako uongee.

## UKIRI WA KINABII

**Mungu wangu atanipa mahitaji yangu yote kulingana na utukufu wake kwa Kristo Yesu. Natembea kwa afya ya kimungu kwa kupigwa kwake nilipona. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 4:13



**Wafilipi 4:13**
**Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.**

Jifunze kukiri jambo hili wakati wote, kwamba unatiwa nguvu kutoka ndani mwako na kupewa uweza wa kufanya miujiza. Hii inamaanisha kwamba uwezo wako hauna kikomo na hakuna jambo ambalo hauwezi kufanikisha.

Kuwa na ujasiri kama Paulo na tamka, 'ninayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu'(wafilipi 4:13). Unaweza kuuliza, "Je, inakuwaje kama ninajisikia goigoi ndani yangu?" Hi ini sababu kuu zaidi ya kusimamia ukiri wako.

Ukishakiri husisubirie ishara kutoka nje. Pokea na anza kutenda kazi na uelewa wa mtu aliewezeshwa. Hivyo ndivyo unachukulia vema tuliopowe na Mungu kupitia injili.

## UKIRI WA KINABII

**Mungu amenijalia kwa kadei ya utajiri wa utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho wake matika utu wa ndani.**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 3:5



**Waebrania 13:5**
**...Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa.**

Ni ahadi ya namna gani tuliyonanyo ndani ya Kristo. Tunao uhakika kwamba yupo nasi wakati wote, msaada wetu wa karibu kwenye matatizo. Benki inaweza kukuangusha, daktari anaweza kushindwa lakini hatokupungukia kabisa, wala kukuacha kabisa!

Tazama, upendo wa Bwana kwako hauna sababu. Hii inamaana kwamba anakupenda leo kama ambavyo alikupenda jana ulipokuwa madhabahuni unampa maisha yako. Hakuna unachoweza kufanya kumaliza upendo wake kwako. Hii ndiyo sababu Daudi aliweza kukiri kiujasiri, "Bwana ndiye mchungaji wangu, sitopungukiwa na kitu"

Haijalishi ni hali gani itasimama kinyume nawe siku ya leo, Mungu yupo pamoja nawe. Na kama Mungu yupo upande wako, uko kwenye upande wa ushindi; hauwezi kushindwa. Hali yeyote uliyonayo unafanikiwa!

## UKIRI WA KINABII

**Siko peke yangu kamwe kwani Bwana yu pamoja nami. Ninayo nguvu ya kushinda kila hali kwani wale walio upande wangu ni wengi kuliko wale waliokinyume nami katika jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 91:15, kumbukumbu la tolati 31:6



**Nia ya Bwana**
**1 Wakorintho 2:16 Maana, Ni nani aliyeifahamu nia ya Bwana, amwelimishe? Lakini sisi tunayo nia ya Kristo.**

Neno la Mungu linasema kwamba tunayo nia ya Kristo. Nia ya Kristo haijazeeka, haiko taratibu wala haisahau! Haijalishi unafika umri gani. Hauhitaji kuwa msahaulifu.

Husiamini wala kukiri kinachozungumzwa na sayansi wala marafiki zako. Amini na kiri neno la Mungu liletalo uhai. Nguvu ya uhai na mauti uko kwenye ulimi wako (mithali 18:21). Hivyo tumia ulimi wako kwaajili ya uhai.

Husikae na kusema "ninazeeka na kuwa msahaulifu." Sema, "ninayo nia ya Kristo. Nia yangu ni yenye wepesi na uhakika kwani ninayo nia ya Kristo!" Amini, kiri, na uone fikra zako na kumbukumbu yako ikiishi kwenye ukiri huo.

## UKIRI WA KINABII

**Ninayo nia ya Kristo. Nia yangu inayo utayari. Siwezi kuchanganyikiwa kamwe, ninajua cha kufanya kila wakati kwasababu hekima ya Mungu inafanya kazi ndani yangu. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 18:21



GoodNews DAILY



**Mathayo 6:33**
**"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake na hayo yote mtazidishiwa.**

Hatutakiwi kutafuta vitu kama ambavyo mataifa hutafuta. Neno "utafuteni" kwenye "mataifa huyatafuta" (mstari wa 32) ni neno la kigiriki epizētéō. Hili linamaanisha kumtafuta kwa nguvu zako zote, kwa jasho jingi na kwa taabu.

Ya lakini vile ambavyo Mungu anataka tumtafute kwenye "utafuteni kwanza ufalme wake" ni neno la kigiriki zētéo, lenye maana kuwa na kiu, na kutamani kuabudu. Hii ni hali ya kuwa na kiu na kutamani ufalme wa Mungu, bila kutenda kazi kubwa ama kutaabika. Warumi 14:17 inatuambia kwamba ufamle wa Mungu ni haki, amani na furaha katika Roho Mtakatifu.

Hivi leo, mtafute Yesu kwanza. Tumia muda pamoja nae na sikiliza neno lake. Unapofanya hivi, yale mambo ambayo unataabika kupata yatazidishiwa kwako bila kazi ngumu. Mungu anao mpango wa tofauti wa kukupatia mahitaji yako na sio namna za dunia hii, bali ni kupitia Ufalme wake.

## UKIRI WA KINABII

**Uwoga, magonjwa, umasikini na mauti hayana sehemu kwangu kwasababu, Ufalme wa Mungu unayo nafasi ya kwanza kwenye maisha yangu. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Mathayo 6:28-35



**Marko 11:23**
**Amin, nawaambia, Ye yote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake.**

Sasa hapa Yesu hakuwa anazungumza lugha ya picha kama ambavyo wengi wangedhania. Kumbuka kwamba kwenye mstari wa nyuma Yesu alizungumza na mti!

Yesu alizungumza na upepo pamoja na bahari, alizungumza na samaki baharini, alizungumza na mwili wa mtu aliyefariki n.k, na vyote hivi vilimsikiliza na kumtii. Wewe pia umepewa uwezo huu wa kusababisha mabadiliko kupitia neno la Mungu kinywani mwako kwani, 'kama Yeye alivyo (Yesu), ndivyo tulivyo na sisi ulimwenguni humu.'

Maneno yako yaliyojaa imani ndiyo yatakayopima ubora wa maisha utakayoishi! Haijalishi hali yako ama mahali utakapojikuta, unaweza kusababisha mabadiliko kwa maneno yako yaliyojaa imani!

## UKIRI WA KINABII

**Bwana, asante kwa neno lako. Ni kweli ambayo ninaiishi leo na kila siku. Kuelewa na kukiri neno lako kumeniweka juu na kunipa ushindi siku ya leo!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 4:17



**1 Wakorintho 10:13**
**Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu ila Mungu ni mwaminifu ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.**

Ushindi wetu juu ya mishale ya adui ni wa uhakika. Hii ndio sababu biblia inaita maisha yetu ya ukristo vita nzuri ya imani. Ni vita nzuri kwasababu ni vita ambayo tunashinda.

Adui anaweza kushindwa kutambua kwamba ni mtego na akatumia nguvu zake kukuponga, hivyo husiteteleke. Kwa kila jaribu na mtihani ambao unakumbana nao, Mungu amekwisha kukutengenezea njia ya kutokea. Unayo nguvu ya kishinda kila jaribu linalokujia.

Halipo jaribu ambalo ni juu ya uwezo wako, kwani jaribu likapo, anakutengenezea njia ya kutorokea. Unao uwezo wa kushinda kila jaribu lijalo kwako siku ya leo.

## UKIRI WA KINABII

**Dhambi haina mamlaka juu yangu, kwani siko chini ya sheria bali natiwa nguvu na neema ya Mungu kushinda kila wakati.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 6:14



**Yohana 5:14**
**Baada ya hayo Yesu akamkuta ndani ya hekalu, akamwambia, Angalia, umekuwa mzima usitende dhambi tena, lisije likakupata jambo lililo baya zaidi.**

Mungu hajakukatalia wema wake ama baraka zake kwasababu ya mabaya ulioyenda. Mungu anakupenda wakati wote, alikupenda hata kabla haujafanya jambo lolote sahihi.

Zingatia kwenye andiko letu la leo, Yesu anamponya mwanamume aliyekuwa na ugonjwa miaka thelasini na nane. Huyu mwanaume alikuwa mtenda dhambi kwasababu maagizo ya Bwana yalikuwa 'husitende dhambi tena'

Mungu hatumii magonjwa kuwanyenyekeza ama kuwaadhibu wana wake. Ninaamuru Magonjwa, kila aina ya kansa, kila ugonjwa wa damu, kila roho ya udhaifu kukuachilia sasa katika jina la Yesu! Pokea uponyaji katika jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Nimepona katika jina la Yesu! Magonjwa na udhaifu hauna sehemu maishani mwangu. Mimi ni hekalu la roho mtakatifu. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Petro 2:24



**Yakobo 1:25**
**Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.**

Sheria kamilifu ya uhuru ni neno la Mungu, habari njema. Linabeba uweza wa kukuweka huru kwenye kila eneo la maisha yako. Biblia inasema kwamba linaukali kama panga ikatayo kuwili, li hai na lenye nguvu.

Tazama, neno unalopokea hata sasa litakupeleka viwango vingine ndani ya Mungu. Linalo uwezo wa kukubadilisha kutokea ndani mpaka nje. Nguvu ya kubadili maisha yako iko kwenye injili. Inashangaza vile ambavyo Mungu amekwisha tengeneza njia kwaajili ya mimi na wewe kuwa vile alivyotuita kupitia habari njema!

Unapandishwa kutoka utukufu hadi utukufu unavyoitazamia sheria kamilifu iliyo ya uhuru siku ya leo.

## UKIRI WA KINABII

**Kristo anaumbika ndani yangu ninavyoendelea kuitazamia sheria kamilifu iliyo ya uhuru. Ninatolewa utukufu hadi utukufu!**

**SOMO LA ZIADA**
Wagalatia 4:19



**Hebrews 4:15**
**Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi.**

Bwana Yesu anaguswa na ubinadamu wetu— madhaifu yetu, machozi, masikitiko, maumivu na mengineyo! Hakuna jaribu wala mtihani utakaokimbana nao ambao Yesu hauelewi. Pale ambapo unapitia changamoto hiyo, Yesu anapitia pamoja nawe.

Huyu ndiye muwakilishi uliye naye. Huu ndio upendo wa Mungu ili uweze kisonga kwenye kiti cha neema (sio hukumu) kupata rehema na neema kwenye wakati wako wa uhitaji.

Habari njema ni kwamba anafahamu jinsi ambavyo mambo yamekuwa magumu kwenye ndoa yako na kiasi cha maumivu ambayo huo ugonjwa umekusababishia. Hii ndiyo sababu tunaweza kuleta kila ombu mbele za Bwana tukiwa na uhakika kwamba atatutimizia.

## UKIRI WA KINABII

**Neema ya Mungu yanitosha. Ninaweza kushinda changamoto yeyote ijayo mbele yangu katika jina kuu la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Isaya 53:1-6



**Isaya 33:24**
**Wala hapana mwenyeji atakayesema, Mimi mgonjwa watu wakaao humo watasamehewa uovu wao.**

Kwenye andiko letu la leo, nabii Isaya anaongelea mji wa Sayuni na anatueleza kwamba wakaaji wa mji huo hawatasema, 'ninaumwa'

Anakuelezea kuhusu sehemu ya afya kamilifu. Kwa sisi ambao tumezaliwa upya, tumefanyika kuwa wakazi wa mji huu wa kitukufu wenye afya timilifu.

Siku uliyomfanya Yesu kuwa Bwana wa maisha yako, uliingia mahali panaitwa Kristo, mji wa Sayuni, Yerusalemu ya mbingu. Hivi sasa unayo mamlaka na majukumu ya kusema "Hapana" kwa magonjwa na kukataa kuugua.

## UKIRI WA KINABII

**Nimejongea mlima Sayuni, magonjwa hayana nafasi ndani yangu. Uhai wa Mungu unatembea kwenye kila mshipa ndani yangu na seli mwilini mwangu. Nakataa kuugua katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 5:17



**Mathayo 27:46**
**Na kama saa tisa, Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akisema, Eloi, Eloi, lama sabakthani? Yaani, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?**

Yesu alichukuwa nafasi yako ya kutokuwa na kinga ya kiungu pale msalabani. Kwa mara ya kwanza, aliachilia kinga ya kiungu ili wewe uwe nayo siku zote za maisha yako. Aliichukuwa laana yako pale msalabani ili siku ya leo, unapoichukuwa zawadi yake ya haki, unapokea baraka tuu kutoka kwake.

Yesu alipata hasira yote ya Mungu mwilini mwake kwa mara moja alipochukuwa dhambi zako zote pale msalabani. Hukumu yote na hasira yote ya Mungu ulimwangukia ikizimaliza dhambi zote na kumalizika.

Hivi leo, Mungu hana hasira na wewe. Mwili wa Yesu ulichukuwa yote, dhambi zako, laana zako, hasira ya Mungu na hukumu. Hivyo ishi maisha yako bila kutafajia kuona hukumu, bali wema na baraka ya Mungu!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni haki ya Mungu ndani ya Kristo. Siwezi kulaumiwa na ninao uhuru wa kufurahia baraka za Mungu ndani ya maisha yangu.**

**SOMO LA ZIADA**
Isaya 53:5



**Wagalatia 5:22-23**
**Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi juu ya mambo kama hayo hakuna sheria.**

Andiko letu la leo linasema kwamba tunda la roho ni upendo. Tambua kwamba haijasema matunda ya roho bali ni tunda la roho. Hayo mengine yote yametajwa kukuonesha vile ambavyo hili tunda, ambalo ni upendo, laweza kuoneshwa.

Kutenbea kwenye upendo kunatakiwa kuwa rahisi kwako kwasababu biblia inasema kwamba upendo wa Mungu umekwisha kumiminwa kwenye mioyo yetu. Hii inamaanisha kwamba uwezo wako wa kupenda unatokana na kile ambacho Mungu ameweka ndani yako. Kama unatembea kwenye upendo, basi unatembea kwenye roho, ukiwa na uwezo wa kufahamu kila ambacho Mungu anafanya ndani yako na kwenye mazingira yako.

Hakuna kitakachokushangaza. Utajua namna ya kujibu kila changamoto kwenye uchumi wako, kwenye afya yako na familia yako unapotembea kwenye upendo. Chagua kutembea kwenye upendo na uone tunda la roho kwenye kila ufanyalo leo.

## UKIRI WA KINABII

**Nachagua kuruhusu upendo wa Mungu kunitawala. Sitofungwa na kutokusamehe, ninachagua kupenda. Sitoshangazwa kwenye hali yeyote. Ninaongozwa na roho.**

**SOMO LA ZIADA**
Wagalatia 5:15



**Zaburi 23:1**
**Bwana ndiye mchungaji wangu, sitopungukiwa na kitu.**

Kwenye andiko letu la leo, Daudi anamwita Mungu 'Mchungaji wangu' jina binafsi. Alimjua Mungu kuwa pamoja nae na kiongozi wake maishani. Mungu sio mchungaji tuu, ni 'mchungaji wako'.

Daudi alielewa kwamba yeye hajimiliki mwenyewe na yule ambae anammiliki anamjali vya kutosha kumlinda na kumpatia mahitaji yake. Hakuhitaji kuwaza kuhusu mahitaji yeyote. Alitambua kwamba anae mchungaji ambaye ni mwaminifu kwake kumchunga.

Sasa, hii sio kwaajili ya Daudi kwenye agano la kale, biblia inasema kwamba hamjimiki wenyewe, mmenunuliwa kwa thamani. Ohh haleluya! Kama vile Daudi, wewe pia unaweza kukiri kwamba hautopungukiwa kitu. Mpanga mipango wa kimaajabu ni msaidizi wako maishani. Unakwenda mahali pazuri.

## UKIRI WA KINABII

**Leo, ninatambua kwamba Bwana ni mchungaji Wangu binafsi. Ananiongoza na kunielekeza kwenye mafanikio. Sitokosa lolote jema.**

**SOMO LA ZIADA**
1 Wakorintho 6:19-20



**Marko 16:17**
**Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio kwa jina langu watatoa pepo watasema kwa lugha mpya**

Hakuna jina lenye nguvu kishinda jina la Yesu. Tatizo linapotokea, tambua lipo kimbilio. Hakuna mahali kwengine zaidi ya kwenye jina la BWANA.

Hii ndio sababu biblia inasema kwamba halipo jina lingine lenye uwezo wa kutuokoa. Ipo nguvu ndani ya jina. Haijalishi unachopitia siku ya leo, kama mwana wa Mungu unaweza kuchukuwa madaraka juu ya nguvu za giza katika jina la Yesu.

Hujakosa msaada kwenye hiyo hali unayopitia kwani unayo nguvu ndani ya jina la Yesu kupinga mishale ya adui. Je, unaumwa ndani ya mwili wako? Chukuwa mamlaka katika jina la Yesu, na ugonjwa hautokuwa na la ziada zaidi ya kukuachia.

## UKIRI WA KINABII

**Nachukuwa jukumu la mwelekeo wa maisha yangu. Roho mtakatifu yuko kazini ndani yangu, hivyo mwili wangu unafanywa upya katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Matendo ya mitume 4:12



**Joshua 24:13**
**Nami nimewapa ninyi nchi msiyoitendea kazi, na miji msiyoijenga, nanyi mmekaa humo mnakula matunda ya mashamba ya mizabibu na mizeituni msiyoipanda.**

Mungu ameshaahidi kwamba: 'nami nimewapa ninyi nchi msiyoitendea kazi, na miji msiyoijenga, nanyi mmekaa humo, mnakula matunda ya mashamba ya mizabibu na mizeituni msiyopanda.'

Hajasema 'ninaweza kuwapa' yenye maana kwamba anaweza kuwapa ama hasiwape, amesema, 'nimewapa', ikimaanisha amekwisha kuwapa. Ni suala la muda tu kabla ufunuo ulionao kupitia kazi ya Kristo kukuletea matunda ambayo Mungu amekwisha kukubariki.

Tumaini kupokea kwa namna ya kiungu maishani mwako kwasababu umebarikiwa sana ndani ya Kristo. Yesu alichukuwa nafasi yako ya umasikini msalabani. Hivyo basi acha kutazama ukosefu wa malighafi maishani mwako. Utazame msalaba na unene, "natarajia kutembea kwenye baraka zake zote, kwasababu ya kazi yake kamilifu msalabani"

## UKIRI WA KINABII

**Mambo yote ni yangu! Leo, sitokosa lolote jema, na nitatembea kwenye baraka ya Mungu.**

**SOMO LA ZIADA**
Waefeso 1:3



**Yohana 16:13**
**Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote...**

Mungu hatamani ukimbilie na kutegemea hekima ya ulimwengu. Sasa, hakuna tatizo katika kwenda kwa daktari ama kumshirikisha mshauri wa kifedha, lakini Mungu anahitaji uje kwake kwanza kwaajili ya ushauri na maelekezo.

Andiko letu la leo linasema Roho mtakatifu ni Roho wa kweli na atawaongoza awatie kwenye kweli yote. Mungu yuko tayari kukuongoza na kukupatie hekima unayo hitaji kwenenda kwenye maisha yako. Ukiwa na Mungu, hakuna lisilowezekana kwako leo!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaishi maisha ya utoshelevu. Mimi ni ishara na maajabu kwani Bwana ni hekima yangu. Hakuna linalonizidi leo katika jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 2:20



**Waefeso 2:6**
**Mungu alitufufua pamoja na Kristo na kutuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu,**

Katika Ukristo, hatujaitwa kupigana na ibilisi. Shetani, Ibilisi, ni adui yetu, lakini ameshindwa tayari! Amehukumiwa, na sisi ndio tuliopewa jukumu la kutekeleza hukumu yake!

Hivyo, hatupigani naye; tunatoa hukumu ambayo tayari imepitishwa kwake. Ni sehemu ya urithi wetu katika Kristo: "Kutoa hukumu iliyoandikwa-Heshima hii wanayo watakatifu wake wote. Bwana asifiwe! " (Zaburi 149: 9).

Katika Yohana 16:11, Yesu alisema, "mtawala wa ulimwengu huu amehukumiwa." Hiyo inamaanisha Shetani amehukumiwa. Haleluya! Una jukumu la kumweka Shetani mahali pake - chini ya miguu yako! Ndio maana Biblia inasema umtoe nje! Haugombani na Shetani; mtoe tu nje.

## UKIRI WA KINABII

**Hakuna silaha iliyowekwa dhidi yangu itafanikiwa. Hakuna ubaya utakaonipata. Elfu kumi wataanguka mkono wako wa kulia, lakini hautakukaribia wewe, kwa jina la Bwana Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 149:9, Yohana 16:1



**Marko 11:22**
**Yesu akawajibu akawaambia, "Mwaminini Mungu.**

Kwenye andiko letu la leo, tumeambiwa kuwa na imani ya aina kama ya Mungu; imani isiyo ya kawaida ambayo Mungu hutumia. Tunamuona akitumia kanuni hii ya imani katika Mwanzo 1.

Dunia aliyoumba Mungu ilikuwa imeharibiwa na ilifunikwa katika giza kuu. Alitumia imani kuleta ndani ya mwili aliyoyachukua katika ulimwengu wa roho. Kwa kutumia kanuni hiyo hiyo ya imani, unaweza kuunda au kufanya upya ulimwengu wako na kuleta vitu vizuri unavyotaka kuona katika maisha yako.

Uwezo wa kufanya hiki kitokee ni Neno la Mungu kinywani mwako. Hivyo hivyo Mungu alivyoumba ulimwengu kwa kutumia Neno Lake, angalia maisha yako leo. Tumia imani ya aina kama ya Mungu!

## UKIRI WA KINABII

**Roho ya Mungu amenileta mahali penye ustawi wa kudumu ambapo kila kitu kimeamriwa kufanya kazi pamoja kwa faida yangu. Kila ninapokwenda, na katika kila kitu nifanyacho, nafanya maendeleo kwa hatua kubwa.**

**SOMO LA ZIADA**
Waebrania 11:1



**Isaya 53:5**
**Lakini alitobolewa kwa ajili ya makosa yetu, alichubuliwa kwa ajili ya maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.**

Kama unaumwa, jishawishi kuwa Yesu ndiye daktari wako na kwa kupigwa kwake umepona. Hauhitaji kumshawishi Mungu afanye. Yeye si yule anayehitaji kushawishiwa kwa sababu Yeye ndiye mtoaji wa kila baraka.

Ni wewe ambaye unahitaji kushawishiwa kwamba Mungu ameshakupa muujiza wako. Hiyo ndio sababu unakiri Neno lake, kujishawishi, si Mungu, kushawishi moyo wako, si wake.

Unahitaji tu kujishawishi kwamba Mungu anakupenda na anafurahi kukubariki. Jiambie mwenyewe, "Kwa kupigwa kwake mimi nimepona. Sitaangaika na ukosefu. Nimebarikiwa sana, nimependelewa kiasi kikubwa, napendwa sana! " Na umuache Mungu ajumuike na mengineyo.

## UKIRI WA KINABII

**Kristo alichukua kila aina ya magonjwa na maradhi kwenye mwili wake. Matokeo yake, yale magumu zaidi mpaka marahisi hayana nafasi yoyote ndani yangu! Ninaongea na kila shida mwilini mwangu iondoke kwa jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Petro 2:24



**1 Yohana 1:3**
**Twawatangazia lile tuliloliona na kulisikia, ili kwamba nanyi mwe na ushirika nasi. Na ushirika wetu hasa ni pamoja na Baba na Mwanawe, Yesu Kristo.**

Mpaka na isipokuwa utagundua kusudi lako la maisha, haujaishi. Ushirika na Mungu ndio wazo. Ushirika na Mungu sio tu kuwa rafiki yake; sio tu kuwa karibu naye; ni kuwa na umoja naye, kuungana kwa kusudi na nia.

Hilo ndilo jambo kubwa kuliko yote utakaloweza kujua - kuwa katika ushirika na Bwana na kuwasiliana naye kama unayemjua na anayekujua. Hiyo ndiyo sababu ya maisha: kujua kuwa Mungu anakupenda na unampenda na kutembea pamoja naye, kujua ni nini kuwa ndani ya Mungu na Mungu ndani yako.

Jambo kubwa zaidi ambalo mwanadamu angeweza kujua ni kumgundua Yeye,kujigundua mwenyewe ndani Yake, na kumgundua Yeye ndani yako. Chukua mda wa kushirikiana naye leo kwa sababu anakupenda.

## UKIRI WA KINABII

**Nikiwa nashirikiana na Bwana leo, naimarishwa; Napewa nguvu. Aliye ndani yangu ni mkuu kuliko aliye ulimwenguni. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 14:11



**Yohana 3:16**
**"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.**

Wengi ulimwenguni kote hawajui kuwa dhambi zao zimesamehewa. Hakufanya kwa ajili ya Wakristo; Alifanya hivyo kwa ajili ya ulimwengu wote (Yohana 3:16).

Kuna wale ambao leo kwa ujinga hujiweka wenyewe kwenye njia ya adhabu kali. Wanajiadhibu kwa dhambi zao, wakidhani ikiwa wanateseka vya kutosha, Mungu atawahurumia na kupuuzaa dhambi zao. Walakini, haifanyi kazi kwa njia hiyo.

Sio kwa juhudi zako. Kilichohitajika ilikuwa damu isiyo na dhambi, damu ya Yesu Kristo. Yeye pekee ndiye aliyestahili kujitolea mwenyewe kwa ondoleo la dhambi zetu. Haijalishi umekosea nini leo, nina habari njema kwako. Sio lazima kubeba uzito wa dhambi, Alikufanyia hivyo. Unachohitajika kufanya ni kupokea na kunufaika na dhabihu yake, na utakuwa huru kweli!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu; vitu vyote vimekuwa vipya, na nimehesabiwa haki kwa imani. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Waefeso 2:8-9



**Kutoka 12:13**
**Damu itakuwa ishara kwa ajili yenu ya kuonyesha nyumba ambazo mtakuwamo; nami nitakapoiona damu, nitapita juu yenu. Hakuna pigo la uharibifu litakalowagusa ninyi nitakapoipiga Misri.**

Kuna kitu sitaki ukose katika andiko letu la leo. Bwana aliwaambia wana wa Israeli, "nitakapoona hiyo damu, nitapita." Kwa hivyo basi, sifa ya pekee ya Bwana kupitisha nyumba yako katika kambi hiyo ilikuwa ishara ya damu.

Tunajua kiuhalisia kwamba hata kambi ya Israeli, kama jamii nyingine yoyote, ingekuwa na wahusika waliojichanganya huko na umati wa watu wengine. Lakini ikihusu kuwa ni nani atakayeokolewa kutoka kwa ghadhabu ya Mungu, kitu pekee ambacho Mungu alikuwa akitafuta ni damu.

Yesu ni ishara tunayoibeba leo mioyoni mwetu kama waumini. Yeye ndiye sifa ya pekee ambayo Mungu anatafuta kumwokoa kila mwamini kutoka ghadhabu inayokuja. Hii ndio Habari njema tunayohubiri! Mbingu imehakikishiwa kwako. Wewe ndiye haki ya Mungu katika Kristo, haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni haki ya Mungu katika Kristo. Wokovu wangu ni zawadi kutoka kwa Mungu, na hakuna shetani kuzimu awezae kunisogeza. Nimeokolewa kwa neema!**

**SOMO LA ZIADA**
Wagalatia 2:21



**Matahayo 28:18-19**
**Yesu akawajia na kusema, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Kwa sababu hii, enendeni ulimwenguni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu,**

Neno la Kiyunani lililotafsiriwa kama "nguvu" katika andiko letu la leo ni, exousia; inamaanisha mamlaka au utawala. Kabla tu hajarudi mbinguni, alisema, "Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Kwa sababu hii, enendeni.... Sasa angalia. Neno hilo 'kwa sababu' linamaanisha 'kwa sababu hiyo.' Kwa maneno mengine, unaweza kuisoma hivi,

Mamlaka yote nimepewa mbinguni na duniani. Nenda kwa sababu hiyo, na uwafundishe mataifa yote, uwabatize kwa jina ...
Mamlaka yaleyale ambayo Yesu alitumia kukemea dhoruba, kufufua wafu, kutoa pepo, na kuponya wagonjwa ni yetu kutumia sasa. Tumepewa nguvu ya wakili kutumia jina hilo. Hivyo, kukiwa na ripoti katika vyombo vya habari juu ya janga na watu wanaugua, ujue una mamlaka juu ya janga hilo.

## UKIRI WA KINABII

**Kwa mamlaka niliyopewa kwa jina la Bwana Yesu Kristo, hakuna ugonjwa au virusi vitakavyokaribia nyumba yangu kwa jina kuu la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Mathayo 8:5-13



**Hosea 4:6**
**Watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa,**

Ninashangazwa na vitu vyote ambavyo vinaweza kukudhuru kama mwamini, Mungu kwa hekima yake alisema kwamba watu wangu wanaangamizwa kwa kukosa maarifa, ujinga wazi tu. Sio ukosefu wa nguvu, sio hata shetani, ni ujinga wako.

Lakini mshkuru Mungu kwa Habari Njema! Hii ndio sababu Biblia inasema mbadilishwe kwa kufanywa upya akili zenu. Hivi sasa unapoendelea kusoma na kutafakari juu ya Neno hili, ukombozi wako unafanyika. Kuingia kwa Neno Lake huleta nuru. Huwezi kamwe kukosa msaada ukiwa unajua habari njema ya Neno Lake. Unakuwa na mwenye mikakati ya ajabu katika kona yako.

Paulo alisema hatuna ujinga wa vifaa vya adui. Leo, jijumuishe na Habari Njema ya Neno la Mungu. Fedha zako hazitakuwa na chaguo ila kuanguka kwenye mstari. Dhoruba katika ndoa yako italazimika kuisha unapoanza kutembea katika hekima ya Mungu.

## UKIRI WA KINABII

**Sitakuwa mjinga wa ahadi za Mungu katika maisha yangu. Ninapoendelea kusikia Habari Njema ya neema yake. Nageuzwa kutoka utukufu hadi utukufu.**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 4:7



**Wafilipi 4:4**
**Furahini katika Bwana siku zote, tena nasema furahini!**

Katika barua yake kwa Wafilipi, Paulo anawaelekeza wafurahi katika Bwana, na kuonesha umuhimu wa jambo hilo, anajirudia katika sentensi hiyo hiyo. Kwa lugha ya Kiyunani, unapotaka kusema jambo na kuonesha mkazo au umuhimu wake, unajirudia mwenyewe.

Ndio maana unaposoma Injili, baadhi ya taarifa ambazo Bwana alisema zilianza na "hakika, hakika" kuonesha umuhimu wa kile ambacho kilihitaji kusemwa. Gundua anasema, furahini katika Bwana siku zote. Hiyo inamaanisha wakati wote, katika kila changamoto ambayo maisha yanaweza kukutupia, unaweza kuchagua kutunza furaha yako. Ona? Furaha ni chaguo, sio kazi ya hafla, kama furaha.

Huzuni na unyong'ofu hunyonya maisha yako, na matokeo yake ni magonjwa na shida za kiafya. Unahitaji kufurahi kila wakati katika Bwana na uweke msimamo wako wa ushindi. Leo, chagua kucheka kwa sauti kubwa. Unapokutana na changamoto, usiiruhusu kuiba furaha yako kwa sababu ndipo nguvu zako zilipo.

## UKIRI WA KINABII

**Nachagua kufurahi bila kujali kinachotokea hivi sasa! Kuomboleza na huzuni haviko katika msamiati wangu! Nitakuwa na kicheko cha mwisho na kirefu zaidi katika Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 17; 22 Mithali 12:25



**1 Wathesalonike 5:18**
**Shukuruni kwa kila jambo, kwa maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu kwa ajili yenu katika Kristo Yesu.**

Utoaji shukrani hufanya nguvu ya Mungu ianze kufanya kazi katika maisha yako. Angalia maandiko hayasemi mshkuru Mungu kwa kila kitu, lakini kwa kila jambo. Haijalishi maisha yametupa nini kwako, unatakiwa ubaki ukimshukuru Mungu; Kwa kuwa kulia kunaweza kudumu usiku, lakini furaha inakuja asubuhi.

Ikija kwenye vitu ambavyo tunahitaji katika maisha yetu, Mungu anataka tumkaribie kwa mtazamo wa kushukuru kwa kile tunachoomba. Haishangazi?

Kamwe usimridhishe adui kwa kumfanya afikirie amefanikiwa kutatiza siku yako. Ni kupitia shukrani mafanikio yako yalipo!

## UKIRI WA KINABII

**Leo nasimama mshindi katika kila hali nitakayokabili! Sifa yangu ina nguvu ya kuleta muujiza wangu; Sina wasiwasi!**

**SOMO LA ZIADA**
Waefeso 3:20



**2 Petro 1:3**
**Uweza wake wa uungu umetupatia mambo yote tunayohitaji kwa ajili ya uzima na uchaji wa Mungu...**

Mungu ameshafanya kila kitu Alichohitaji kufanya juu ya wokovu wako, afya, ustawi, na kadhalika na amemaliza kazi kabla ya kuweka msingi wa ulimwengu.

Sasa anataka ufaidi vitu vyote unavyomiliki katika Kristo. Anataka uishi katika baraka. Andiko letu la leo linasema, " Uweza wake wa uungu umetupatia mambo yote tunayohitaji kwa ajili ya uzima na uchaji wa Mungu."

Je! Unaweza sasa kuona kwamba hakuna haja ya wewe kuhangaika maishani? Paulo alisisitiza jambo hilo hilo; Alisema katika 1 Wakorintho 3:21, "vitu vyote ni vyako." Kwa kuwa vitu vyote ni vyako, unapaswa kutoka kwenye mahangaiko yote. Kataa maisha magumu. Simama kwenye Neno la Mungu leo - vitu vyote ni vyako - na ushike vilivyo vyako.

## UKIRI WA KINABII

**Maneno yangu si ya kawaida; yamejazwa na nguvu za kimungu, yakitengeneza kile ninachoyatuma yakakamilishe. Ninapoita vitu, vinakuwa. Haleluya! Vitu vyote ni vyangu!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Wakorintho 3:21



**1 Wakorintho 14:14-15**
**Kwa maana nikiomba kwa lugha isiyojulikana, roho yangu inaomba, lakini akili yangu haina matunda. Nifanyeje basi? Nitaomba kwa roho, lakini nitaomba kwa akili yangu pia. Nitaimba kwa roho na nitaimba kwa akili yangu pia.**

Waumini wengi hutumia masaa mengi katika maombi kwa Mungu wakizungumza na ufahamu wao au akili zao. Mtume Paulo anafundisha jinsi alivyokuwa anasali. Ninataka uangalie kwa ukaribu maandiko yanasema nini. Anasema, " Kwa maana nikiomba kwa lugha isiyojulikana, roho yangu inaomba, lakini akili yangu haina matunda."

Subiri kidogo! Kwa hiyo kwa maneno mengine, ikiwa haombi kwa lugha isiyojulikana, roho yake haiombi pia! Hakuwezi kuwa na ukuaji wowote wa kiroho mpaka roho yako iombe. Hitimisho la Paulo kwa jambo hili ni kwamba ataomba na roho na kisha akili pia. Unapoanza kusali kwa Roho, unazingatia sana mafundisho ya Roho Mtakatifu, na utakuwa na ufanisi zaidi katika maombi kuliko unavyoweza kufikiria.

## UKIRI WA KINABII

**Namshukuru Mungu kwamba ninapoanza kuomba kwa roho, maisha yangu ya maombi hubadilishwa, na nguvu kubwa ya kuleta mabadiliko hupatikana. Naweza kumfanya shetani akimbie kwa nguvu ya Roho Mtakatifu kwa jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Yuda 20, Warumi 8:26



**Mithali 10:22**
**Baraka ya BWANA hutajirisha, wala haichanganyi huzuni.**

Kama mtoto wa Mungu unapaswa kufurahia utimilifu wa baraka zake. Andiko letu la leo linasema kwamba baraka hutajirisha, wala haichanganyi huzuni. Hiyo inamaanisha kwamba unapojikuta unateseka, Mungu sio chanzo cha maumivu yako.

Biblia inasema kwamba mwizi ndiye anayekuja kuiba, kuua na kuharibu. Uchungu na hasara uliyopata sio sehemu ya baraka na mpango wa Mungu kwa maisha yako. Biblia inasema Yeye hutajirisha, na haongezi huzuni.

Hiyo inamaanisha kuwa unaweza kufurahia utimilifu wa baraka leo na kukataa kuruhusu mateso yoyote kutoka kwa adui. Mungu anataka uwe tajiri! Hiyo ndiyo kusudi la baraka zake, na haongezi shida yoyote nayo. Ufanisi ni urithi wako!

## UKIRI WA KINABII

**Natembea katika baraka za Mungu; familia yangu ina amani, biashara yangu inafanikiwa kwa jina kuu la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 10:10



**Yohana 12:24**
**Amin, amin nawaambia, mbegu ya ngano isipoanguka ardhini na kufa, hubakia kama mbegu peke yake. Lakini ikifa huzaa mbegu nyingi.**

Hekima ya ulimwengu ya uchumi inatuambia kwamba lazima uhifadhi ili utajirike, lakini Biblia inaelekeza upande mwingine. Usinielewe vibaya sisemi kwamba ni vibaya kuwa na hifadhi yoyote. Hapana kabisa.

Lakini kama andiko letu la leo linavyosema, isipokuwa utatupa mbegu yako na ife, inabaki peke yake. Haijalishi hitaji lako ni kubwa kiasi gani au kama unaomba kwa dhati. Usipotoa kile kilichopo mikononi mwako, hakiwezi kuongezeka.

Mungu anapozungumza na wewe juu ya mbegu, ana mavuno akilini. Usijifanye feki mpaka ufanikiwe kwasababu unaweza usifanikiwe kabisa. Unapopanda mbegu, hakika utafanikiwa. Tunapoongelea juu ya mbegu, si pesa tu. Mda wako ni mbegu, tabasamu lako ni mbegu; wewe ni ghala la mbegu. Kwa hivyo amua kuwa mpanzi leo, na unaweza kuamuru wakati wa mavuno yako!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mpanzi, na Mungu ni mwaminifu kuzidisha kila mbegu iliyopandwa. Ninavyopanda leo, familia yangu imebarikiwa, mavuno yangu yapo karibu, na nitavuna kwa furaha. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Wagalatia 6:7-9



**Warumi 4:21**
**Huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi.**

Andiko letu la leo linatueleza kwamba Abraham hakuwa mdhaifu, bali akiiona ahadi ya Mungu hakusita mkwani aliamini kwamba Mungu anao uwezo wa kufanya yale aliyoahidi.

Ukiangalia mstari unaofata utagundua kwamba, hili ndilo lililomfanya Abraham kuwa mwenye haki. Haikujalisha ni namna gani aliishi na majirani zake, ilihusisha vile ambavyo aliamini ahadi ya Mungu. Kwa lugha nyingine, Mungu alipoona vile ambavyo Abraham anaamini kwamba Mungu anao uwezo wa kufanya yote aliyoahidi, basi akasema huyu ndio mwenye haki.

Kitu pekee kitakachokufanya ustahili baraka ya Bwana ni kumuamini. Hili pekee linakupa haki na kukuweka mahali pa baraka yake kamilifu. Ule uhakika kwamba; unamkiri Kristo unakufanya mwenye haki na kukupa kibali cha baraka za Mungu.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mwenye haki wa Mungu ndani ya Kristo. Nimebarikiwa na kila baraka kwenye ulimwengu wa roho ndani ya Kristo Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 5:21



GoodNews DAILY



**Yohana 1:14**
**Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba amejaa neema na kweli.**

Kipindi ambacho Yesu alikuwa anatembea ulimwenguni, alikuwa katika hali ya utukufu wa upendo kamili wa Mungu kwa viumbe vyake. Andiko letu la leo linasema kwamba amejaa neema na kweli.

Sasa, hata kama Bwana hatembei nasi tena katika mwili, ninayo habari njema kwako. Lile neno ambalo lilifanyika kuwa mwili kipindi cha muduma yake duniani, halijapungua nguvu na neema hata kidogo. Bado unao uwezo wa kushiriki na Bwana Yesu kupitia neno lake.

Kama unahisi ulimwengu wote umesimama kinyume nawe, neno lake linasema hatokupungukia wala hatokuacha kabisa. Je, unaumwa mwilini mwako hivi leo? Neno lake linasema kwa kupigwa kwake tumepona. Haijalishi unachohitaji hivi leo, neema yake yakutosha. Unapolotazama neno siku ya leo, unapokea neema ya kuvunja ulevi na tabia zingine, pamoja na mioyo iliyovunjika katika jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Neema ya Mungu yanitosha. Ninaweza mambo yote kupitia Kristo anitiaye nguvu. Aliyeko ndani yangu ni mkubwa kuliko aliyeko ulimwenguni. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8:3-4



**Zekaria 4:6**
**Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi.**

Kama vile ambavyo tunaweza kujaribu kutenda makuu kupitia nguvu zetu za kibinadam, inakuwa ngumu. Huu haukuwa mpango wa Mungu. Ametupatia Roho wake ambae ni mwenye nguvu kupita yote ulimwenguni.

Tunaweza kufanya makuu tunapoweza kuungana na ile nguvu iliyoko ndani yetu. Hii inatuambia kwamba kama yule yule roho aliyemfufua Kristo katika wafu, ataihuisha miili yenu kwa Roho wake akaaye ndani yenu.

Unachohitaji kutembea kwenye ushindi ni Roho Mtakatifu. Ni mwandishi wa yote mema maishani mwako, hatoacha jambo, haja yake kwako ni kukuona ukifikia uwezo wako wa juu.

Mtambue katika kila ufanyalo. Mruhusu awe anaekuongoza kwenye kila kitu ufanyacho hivi leo.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mwana wa Mungu, niliyejaa nguvu na roho mtakatifu. Ninayaweza yote kupitia Kristo anitiaye nguvu katika jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8:11



**Mithali 23:7**
**Maana aonavyo nafsini mwake, ndivyo alivyo. Akuambia, Haya, kula, kunywa Lakini moyo wake hauwi pamoja nawe.**

Husidharau nguvu ya mawazo yako, ni zaidi ya picha zisozokuwa na maana. Mawazo ni picha za fikra na zinabeba nguvu ya kujenga ama kubomoa. Wewe ndiye unayeunda mawazo yako, mawazo ni maumbo ya vifra yatokanayo na picha kwenye fikra zako. Mawazo ya mwanadamu yakiwekwa kazini vibaya, yatamuweka kwenye kifungo na katika upande mwingine, yatamletea uhuru.

Kama umeyachoka maisha unayoishi, badilisha mawazo yako. Maisha yako yanaenenda kwenye upande wa mawazo yako. Vile ambavyo mawazo yako yalivyo, yanaunda maisha yako. Wewe ni picha ya mawazo yako.

Kama unataka maisha ambayo Mungu amekupangia, fananisha mawazo yako na neno la Mungu na maisha yako yatakuwa matokeo ya neno.

## UKIRI WA KINABII

**Leo ninaweka kazini nguvu ya mawazo yangu. Najiona nikiwa kiongozi sokoni. Ninawaza fursa, maisha yangu yatakuwa ushuhuda wa Mungu myenda maajabu katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Waefeso 3:20 Wafilipi 4:8



**Wakolosai 2:15**
**akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo.**

Andiko lililopo hapo juu linaonesha kwamba tunao uhakika wa ushindi juu ya enzi na mamlaka. Ushindi wetu hautokani na yale tunayotenda ama yale ambayo tunatenda. Ushindi wetu unatokana na yale ambayo Bwana na Mwokozi wetu amekwisha fanya. Yesu alizivua enzi na mamlaka! Neno kuzivua letafsiriwa kutoka kwenye kigiriki apekŷomai lenye maana ya kuondoa ngao na faida yote kutoka kwa mtu. Aliwafanya wasiwe kitu chochote kwenye suala ya kututawala.

Alifanya maonesho hadharani ya ibilisi na mapepo yake. Hawewezi kukutawala tena kiuchumi. Hizi nguvu hazipo. Ni nguvu zisizo na enzi. Hatujaribu kuwashinda, kubali kwa imani kile ambacho Yesu alifanya. Kile alichofanya, alifanya kwaajili yako! Ushindi wa Kristo ni ushindi wako. Katika familia yako, Kristo amekwisha shinda. Dai ushindi huu juu ya ibilisi katia uchumi wako, ndoa yako na afya yako.

Haijalishi ni changamoto gani unapitia, hivi leo habari njema ni kwamba, Kristo ameshinda. Adui ameondolewa uweza na wewe unaweza kuchukuwa ushindi. Anza kufanyia mazoezi mamlaka yako ndani ya Kristo na ufufahie ukamilifu wa baraka za Mungu siku ya leo.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi siko chini ya ibilisi na jeshi lake. Nimefichwa ndani ya Kristo na nimewashinda, aliyeko ndani yangu ni mkubwa kuliko yule aliye ulimwenguni.**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 4:4



**1 Yohana 5:4-5**
**Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu. Mwenye kuushinda ulimwengu ni nani, isipokuwa ni yeye aaminiye ya kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu?**

Mwanamume ama mwanamke amwaminie Yes uni mshindi. Kwa hakika, amezaliwa kwaajili ya ushindi. Kwenye andiko letu hapo juu tunaelewa kwamba yeyote aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Anayo amira ndani yake kwaajili ya kufurika. Haijalishi kitakachomtokea, atakuwa mshindi. Umeumbwa kwaajili ya ukuu na utukufu. Umeushinda ulimwengu.

Mungu alizijua changamoto zilizokuwa zinakuja ulimwenguni, na akaumba mwanadamu mwenye uwezo wa kushinda changamoto zote. Huyu mwanadamu ni kiumbe kipya. Yesu Kristo amekupa maisha ya ushindi, kataa chochote tofauti.

Neno la Mungu linasema, wewe ni zaidi ya mshindi, wewe ni mzawa wa Mungu na ushindi uko ndani ya DNA yako. Enenda ukashinde katika jina la Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Nimeubwa kushinda. Sishindani bali ninatawala katika jina la Yesu. Nimeushinda ulimwengu; imani yangu ndiyo ushindi, na ninashinda kila siku.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8:37



**Waefeso 3:19**
**na kuujua upendo wake Kristo, upitao ufahamu kwa jinsi ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu.**

Kujawa na Mungu ni kujawa na vile ambavyo Mungu yu nawe na mambo yote aliyonayo kwaajili yako. Kujawa na Mungu ni kufika kwenye mahali pa afya, uhai, amani, utoshelevu na usawa. Mungu alipokuumba, alikuumba kuenenda katika ubora wa hali ya juu kabisa kama ambavyo unakuwa umewekeza aina sahihi ya mafuta ama petroli.

Unapotambua ni kihasi gani Mungu anakupenda na ukajijaza kutokana na upendo huo, utajazwa na ukamilifu wa Mungu katika namna ya kiungu. Biblia inatuambia kwamba Mungu ni pendo. Unapokuwa na ufahamu wa pendo lake kwako, unaanza kutembea katika hali ya kiungu.

Kaka zangu na dada zangu, unapoanza kutembea kwenye upendo, utaanza kuona baraka tele za Mungu zinifunguka maishani mwako, utavutia baraka.

## UKIRI WA KINABII

**Upendo wa Mungu umekwisha kumiminwa kwenye moyo wangu katika jina la Yesu. Nakataa kutembea kwenye uwoga na hukumu, ninakubalika kwenye wapendwa, haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 4:8,16



**Mithali 22:6-7**
**Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee. Tajiri humtawala maskini, Naye akopaye ni mtumwa wake akopeshaye.**

Hili ni andiko ambalo linawachanganya wengi lakini ukilitazama kwa umakini, kila kitu kipo hapo kwenye maandiko. Tumekuja na mafundisho ya kila aina kutoka kwenye andiko hili wakati majibu yapo kwenye mstari unaofuata.

Tajiri humtawala maskini, naye akopaye ni mtumwa wa akopeshaye. Ndivyo hivyo! Hicho ndicho tunatakiwa kuwalea watoto wetu. Kuwaeleza ya kwamba wanatakiwa kuwa watoaji na sio wapokeaji. Wao ni kichwa na sio mkia. Tazama, mwanamume kwenye haki huacha urithi kwaajili ya watoto na wajukuu wake.

Haya ndiyo mambo tunatakiwa kufundisha vizazi vijavyo. Tumeitwa kuwezesha kizazi kijacho na kuacha urithi wa kimungu kwaajili yao. Jinsi tuwaleavyo watoto wet uni juu yetu, lakini biblia inatuonesha ni mambo gani ya kutia mkazo.

## UKIRI WA KINABII

**Watoto wangu hawatokosa ama kukumbwa na njaa navyowafunza kila mara njia za Mungu. Wametiwa nguvu kufanikiwa na hawatoondoka kwenye urithi wao.**

**SOMO LA  ZIADA**
Mithali 4:5



**Wagalatia 5:6**
**Maana katika Kristo Yesu kutahiriwa hakufai neno, wala kutokutahiriwa, bali imani itendayo kazi kwa upendo.**

Imani hutenda kazi kwa upendo. Mkristo anaporuhusu wivu wenye uchungu na ugomvi ndani ya moyo wake, imani yake yaweza kusogeza milima, lakini haitomtukuza Mungu kwasababu hatembei kwenye upendo. Kulingana na Yakobo 3:16, wivu na ugomvi ndipo palipo machafuko, na kila tendo baya.

Warumi 10:17 inasema, "imani huja kwa kusikia na kusikia kwa neno la Mungu." Imani yenye kuweza kubadilisha ulimwengu huja kwako kwa neno la Mungu. Lakini machafuko na kila tendo baya laweza kuzuia lile neno la Mungu linalotakiwa kuikuza imani yako, kulichafua na kulifanya lishindwe kutenda.

Fanya maamuzi siku ya leo kukataa kuwa na uchungu na kuwa mwepesi kusamehe waliokuudhi. Kataa kuwa na kisasi na mtu yeyote na imani yako itaanza kutenda. Unakuwa mshindi leo.

## UKIRI WA KINABII

**Nachagua kuachilia maudhi yote na kutembea kwenye upendo. Sina uchungu; niko huru kupenda katika jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Waebrania 12:15



**2 Wakorintho 4:18**
**tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu bali visivyoonekana ni vya milele.**

Kwenye andiko letu la leo, neno la kiyunani lililotafsiriwa 'angalia' linamaanisha kuzingatia, kuweka alama, na kutambua andiko. Kwahiyo, inamaanisha husizingatie, husiweke alama na husitambue changamoto ama vikwazo utakavopitia kwenye vita vyako vya imani. Mbadala, tazama kila changamoto kama mkate.

Tazama kila changamoto kama ngazi ya kukuinua, kwani hakuna litakalo fanikiwa kusimama kinyume nawe kwasababu wewe ni zaidi ya mshindi. Isaya 54:17 inasema kila silaha ifanywayo juu yako haitashinda. Leo zitazame hali zako ambazo zinaonekana kama haziwezekani kama sehemu ya kujipatia ushuhuda. Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Ninaweza mambo yote kupitia yeye anitiaye nguvu. Hakuna linaloshindikana kwangu. Mimi ni zaidi ya mshindi!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8:37



**Marko 6:51-52**
**Akapanda mle chomboni walimo upepo ukakoma wakashangaa sana mioyoni mwao kwa maana hawakufahamu habari za ile mikate, lakini mioyo yao ilikuwa mizito.**

Biblia inasema kwamba wanafunzi walipomuona Yesu anatembea kwenye maji walishangaa sana mioyoni mwao. Wasingeweza kuamini bila kuona kwa macho. Hapa hata wewe utakubi kwamba jambo hili lilikuwa la kustahajabisha na hawakuwa wameona jambo kama hilo.

Ila tazama mstari unaofuata, unasema, "hawakufahamu habari za ile mikate, lakini mioyo yao ilikuwa mizigo." Kwenye fahamu za Mungu, hawakutakiwa kustahajabu kumuona akitembea kwenye maji. Laiti kama wangeelewa kwamba muujiza wa mikate ulikuwa mkubwa zaidi, wangelijua kwamba ni rahisi kwa Bwana kutembea kwenye maji. Ila anasema mioyo yao ilikuwa migumu.

Hii ndio sababu maandiko yanatusihi kutokusahau fadhira zake na kuwa wenye shukrani kwenye kila jambo, hasahasa tunapofanya maombi yetu kwa Mungu. Unaweza kusogea hatua nyingine kwenye maisha yako unapochagua kutambua kila muujiza ambao Mungu amekutendea.

## UKIRI WA KINABII

**Ninashukuru kwaajili ya mambo yote makuu yaliyotendeka kwenye maisha yangu kupitia Kristo, na ninapokea hatua ya juu kiroho kuona vile ambavyo wengine hawawezi kuona katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Marko 6:51



**Warumi 4:20**
**Lakini akiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu**

Biblia inasema tufuate hatua za imani za baba yetu Abraham. Hakusita kwenye imani. Nataka uone kwamba biblia inasema, "hakusita kwa KUTOKUAMINI." Hii inamaanisha kwamba Abraham alikuwa na ahadi ya Mungu kwanza kwa kile alichokuwa amashikilia.

Watu wengi hudai, "sitougua, hilo gari ni langu, hiyo kazi ni yangu, hiki na kile ni changu." Lakini mwishoni, wanaishia kuwa na msongo wa mawazo wanaposhindwa kuona vile walivyokiri. Hi ini kwasababu wanasema kile wanachotamani badala ya kusimama kwenye neno la Mungu ambalo linawaahidi vile vitu wanavyokiri.

Matumizi ya neno "ahadi" kwenye Warumi 4:20 linamaanisha uhakika wa Mungu, dhamana ya Mungu kwa Abraham, ama kiapo cha Mungu. Chochote unachopitia leo, shikilia ahadi ya Mungu kwani yeye ni mwaminifu kukutimizia.

## UKIRI WA KINABII

**Neno la Mungu ndiyo usemi wa mwisho kwenye maisha yangu. Sitosita kwenye ahadi za Mungu. Hakuna kiasi cha changamoto zitakazoniyumbisha. Nabaki mwenye nguvu ndani ya neno katika jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Yoshua 1:5-8



**2 Wakorintho 5:17**
**Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya…**

Hivi unafahamu, ile dakika uliokoka ulifanyika kuwa mwanadamu mpya? Kila jambo ulilofanya kabla na vile ambavyo watu walikujua haipo tena. Wewe ni kiumbe kipya hasiyekuwa na historia ya nyuma.

Hi ini habari inayostahili sifa, habari nzuri sana. Ni kama vile haujawahi kuiba, ama haujawahi kwenda jela. Tazama, Bwana ametengeneza makazi yake ndani ya moyo wako na amekupa roho mpya. Hii inamaanisha amakufanya mwenye haki, hasiye na hatia wala lawama. Mungu anakutazama na anamuona Yesu kwenye nafasi yako. Ghafla, umekuwa kiumbe kipya ambae hakuwahi kuwepo.

Leo, tembea kwenye mwanga wa hii kweli na kataa ibilisi ama mtu mwingine yeyote kukufanya ujisikie vinginevyo. Wewe huna dhambi wala aibu, hii ni kweli ikuwekayo huru. Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni kiumbe kipya ndani ya Kristo ambaye sijafungwa na mambo ya nyuma. Neema yake imenipa neema ya maisha, na ninatembea kwenye mwanga wa ukombozi wake na upendo.**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 3:4



**Wakolosai 2:10**
**Na ninyi mmetimilika katika yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka.**

Unaona nini unapojitazama? Je, unaona mtu mwenye mapungufu ? Je, unaona makosa yako ya zamani na mapungufu kwenye sehemu nyingi za maisha yako? Ama unaona mtu aliyekamilika ndani ya Kristo?

Habari njema ni kwamba Mungu haoni kama ambavyo mwanadamu anaona. Mwanadamu anaona mwili, Mungu anaona roho. Anatuona wakamilifu ndani ya Kristo. Pamoja na mapungufu yetu, anatuona kama viumbe vipya, washiriki wa namna yake ya kiungu, na zaidi ya washindi juu ya makosa yetu. Na anataka tunione kama vile atuonavyo yeye.

Chochote inachoweza kuhisi umepungukiwa, iwe ni tabia ya kiungu ama afya ya mwili, amani kwenye familia yako ama uhuru wa kifedha, tunayo yote ndani ya Kristo. Hauvipati baadae, unavyo hata sasa. Ndiyo maana Yohana anasema, "sasa sis ini wana wa Mungu." Hatusubirii; tumeshakuwa. Yesu ni msamaha wako kamili, haki yako kamili, kibali chako kamili, na ulimzi wako kamili.

## UKIRI WA KINABII

**Bwana ni nguvu yangu na mwimbo wangu, na amekuwa mkombozi wangu. Mimi ni kamili ndani ya Kristo bila lililovunjika ama kupotea.**

**SOMO LA ZIADA**
2 Petro 1:4



**Zaburi 46:1**
**Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso.**

Hivi unafahamu kwamba uwoga hautokuwa na mahali ndani ya akili yako pale utakapokiwa na ufahamu kwamba hatokupungukia wala kukuacha kabisa? Ametuahidi kupitia neno lake kwamba, kama alivyokuwa na Musa pamoja na manabii, atakuwa nasi pia. Ukweli wa kuubwa upya ni kwamba anaishi ndani yetu! Utamuona akiongeza furaha na kukustawisha katika kila usemalo na ufanyalo!

Kama uko katikati ya mabishano, unamuona Bwana amesimama kando yako. Maneno yako yatabadilika, na lugha yako ya mwili itakuwa ya suluhisho zaidi pale utakapomuona amesimama pamoja nawe, akikupatia neema. Pataliwepo na cha kukuzuia ambacho hakijazaliwa kwa nguvu ya nia, bali uweza wa kiungu pale utakapofahamu kwamba yule akupendaye na akilindae yu pamoja nawe.

Husikubali kupoteza ujasiri wako pamoja na furaha yako. Kumbuka, Bwana yu pamoja nawe siku zote, na hakuna changamoto inayokuja kwako ambayo hawezi kuishinda. Furahia maisha ukitambua kwamba unalindwa na Mungu. Hatokupungukia wala kukuacha kabisa.

## UKIRI WA KINABII

**Mung uni msaada wa karibu wakati wa uhitaji na ananifanya nashinda kila hali. Siwezi kushindwa kwani Mungu yu upande wangu katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Yoshua 1:5, Matayo 28:4



**Kumbukumbu la Torati 28:4**
**Utabarikiwa uzao wa tumbo lako…**

Ni kweli Mungu alisema, "utabarikiwa uzao wa tumbo lako." Hakuwa anamaanisha watoto wako pekee kwani ingalikuwa hivyo angesema, "watabarikiwa watoto wako." Hapana, Mungu alimaanisha kila kitokacho mwilini mwako kitabarikiwa. Kila kitu cha mwilini na kitokacho mwilini mwako kitakuwa cha kiwango cha juu.

Hii inajumuisha afya yako. Kwahiyo hata kama daktari amesema unahali fulani mwilini mwako ambayo sio ya kawaida, amini ya kwamba Mungu anaiita afya yako, ambayo ni uzao wa mwili wako, umebarikiwa. Tegemea kutembea kwenye afya ya kiungu kila mara!

Kaka zangu na dada zangu, nataka muelewe kwamba mlikuwa mmebarikiwa hata kabla ibilisi hajajaribu kuwalaani. Hamuwezi kulaaniwa. Kila kitu kitokacho kwenu hakicharibu kupata baraka, kimeshabarikiwa! Utabarikiwa uzao wa tumbo lako!

## UKIRI WA KINABII

**Nimefanywa kamili mwilini mwangu. Roho wa Mungu ndani yangu ananipa rutuba na nguvu kila siku katika jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8:11



**Wafilipi 4:19**
**Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.**

Nimesikia watu wengi wakiomba mstari huu bila kuwa na uelewa pamoja na ufunuo. Tunatakiwa kuelewa huu mstari kulingana na mtazamo wa mwandishi. Chukuwa muda kutafakari ni jambo gani limemfanya mwandishi kuandika alichoandika.


Kwanza, hi ini barua kutoka kwa mtume Paulo kwaajili ya kanisa lililokuwa filipi. Kanisa lilielewa umuhimu wa kusaidia huduma mpaka mtume Paulo akasema, kwasababu ya ushiriki wao, Mungu wake na akatumizie mahitaji ya washiriki wote. Umeona hilo?

Unapokuwa mfadhili wa ufalme, hauwezi kukumbana na ukosefu maishani mwako, iwe kifedha, kwenye afya ama mahusiano. Kwani Mungu ameshaandaa vyote unavyohitaji kwa vingi, neema yake tele! Kama nabii wa Mungu, ninakiri na kutamka kila hitaji kwenye maisha yako kutimizwa katika jina la Yesu. Kuna utajiri ndani ya Kristo, upokee sasa!

## UKIRI WA KINABII

**Bwana ndiye mchungaji wangu, sitopungukiwa na lolote jema. Ninajazwa kutoka juu; ninamtumikia Mungu wa zaidi ya utoshelevu.**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 6:9


Uebert Angel
Available NOW!
hello
Holy Spirit
ORDER NOW AT
WWW.UEBERTANGEL.ORG

OSBORN INSTITUTE of THEOLOGY


Osborn Institute of Theology (OIT), fully accredited by Transworld Accrediting Commission International provides an award-winning online learning platform that equips men and women with the revealed Word of God. OIT prepares men and women to share and bear witness of Jesus Christ to the Church and the World.

ACADEMIC EXCELLENCE
TRANSWORLD ACCREDITING COMMISSION INTERNATIONAL
EDUCATION ACCOUNTABILITY



ENROL NOW!

www.osborninstitute.com


UEBERT ANGEL
Bestselling Author of Supernatural Power of the Believer
AVAILABLE NOW
SPIRITUAL
WARFARE
How To Enforce Your God-given Supernatural Authority
to Neutralise Demonic Activity, Overcome Demonic Strategies
AND PULL DOWN STRONGHOLDS
AN EXPOSÉ of SATAN'S LIES and TRICKERY
ORDER NOW AT
WWW.UEBERTANGEL.ORG



**Yohana 1:14**
**Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli.**

Bwana Yesu alipokuwa akitembea hapa duniani, alikuwa ni dhihirisho na muonekano kamili wa upendo wa Mungu kwa uumbaji wake. Andiko letu la leo linasema kwamba alikuwa amejaa neema na kweli. Sasa, hata kama Bwana hatembei tena kati yetu kimwili, nina habari njema kwako.

Neno hilo hilo ambalo lilikuwa mwili katika siku za huduma ya kidunia halijapoteza hata unzi moja ya nguvu na neema. Bado unaweza kuuona utu wa Bwana Yesu na kuelewana naye kupitia neno lake. Ikiwa unahisi ulimwengu wote uko kinyume na wewe hivi sasa, Neno lake linasema kwamba hatakuacha kamwe. Je! Wewe ni mgonjwa katika mwili wako leo? Neno lake linatangaza kwamba "kwa kupigwa kwake, mliponywa."

Haijalishi unahitaji nini leo, neema yake inatosha kwako. Unapoangalia ndani ya Neno la Mungu leo, neema inaandaliwa kuvunja kila kero, kuponya kila moyo uliovunjika kwa jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Neema ya Mungu inatosha kwangu. Naweza kufanya vitu vyote kupitia Kristo anayenitia nguvu! Yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yeye aliye ulimwenguni. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8:3-4



**Zekaria 4:6**
**Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho yangu, asema Bwana mwenye Nguvu zote.**

Kwa kadri tunavyoweza kujaribu kufanya unyonyaji mkubwa kupitia nguvu zetu za kibinadamu, daima tunapambana. Hii haikuwa kamwe mpango wa Mungu. Ametupa Roho yake ambaye ndiye kiumbe hodari zaidi ulimwenguni.

Tunaweza kufanya unyonyaji mkubwa tunagusa nguvu za Mungu ndani yetu. Biblia inatuambia kuwa ikiwa Roho ya Yeye aliyemfufua Kristo kutoka kwa wafu anakaa ndani yenu, Yeye aliyemfufua Kristo kutoka kwa wafu atahuisha miili yenu pia inayokufa kwa Roho wake anayekaa ndani yenu.
Unachohitaji kutembea kwa ushindi ni Roho Mtakatifu. Yeye ndiye mwandishi wa yote ambayo ni mazuri maishani mwako, na Yeye habanii kamwe chochote kizuri kutoka kwako. Matamanio yake ni wewe kuzaa na kufanikisha uwezo wako mkubwa. Mjulishe katika njia zako zote. Acha Yeye awe anayekuongoza katika kila kitu unachofanya leo.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mtoto wa Mungu nimejaa Roho Mtakatifu na nguvu. Naweza kufanya vitu vyote kupitia Kristo anayenitia nguvu kwa jina kuu la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8:11



**Yohana 5:14**
**Baadaye Yesu akamkuta yule mtu aliyemponya ndani ya Hekalu na kumwambia, "Tazama umeponywa, usitende dhambi tena. La sivyo, lisije likakupata jambo baya zaidi."**

Tofauti na yale ambayo wengi wamefundishwa na kuamini, Mungu habanii uzuri wake au baraka zake kwa sababu ya makosa yoyote ambayo unaweza ukawa umefanya. Mungu ni mwema wakati wote. Yeye hana mabadiliko ya kihemko na Alikupenda na kukubariki muda mrefu kabla haujafanya chochote sahihi.

Angalia katika andiko letu la leo, Bwana Yesu amemponya mtu ambaye amekuwa mgonjwa kwa miaka thelathini na nane na jambo la kufurahisha ni kwamba mtu huyu ni wazi kuwa ni mdhambi maana maagizo ya Bwana yalikuwa "usitende dhambi tena." Najua ulikosa ufunuo hapo hapo. Bwana Yesu hakusubiri mtu huyo atubu kabla ya kunyoosha mkono wake kumponya.
Mungu hatumii ugonjwa kuwanyenyekeza au kuwaadhibu watoto wake. Huo ni uwongo kutoka shimo la kuzimu. Na ikiwa wewe ni mgonjwa katika mwili wako leo, nataka uweke mkono wako maumivu hayo yaliko. Ninazungumza kwa mamlaka ya Roho Mtakatifu, naamuru magonjwa, kila aina ya saratani, kila ugonjwa wa damu, kila roho ya udhaifu iachane na mwili wako sasa kwa jina kuu la Yesu! Ponywa kwa jina kuu la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Nimepona kwa jina la Yesu! Maradhi na magonjwa hayana nafasi ndani yangu, mimi ni Hekalu la Roho Mtakatifu, haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Petro 2:24



**Wakolosai 2:15**
**Mungu akiisha kuzivua enzi na mamlaka, alizifanya kuwa kitu cha fedheha hadharani kwa kuziburura kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba wa Kristo.**

Andiko la hapo juu linathibitisha zaidi ya kivuli cha mashaka yoyote kuwa tuna ushindi juu ya wakuu wote na nguvu zote. Ushindi wetu si kutokana na kile tulichofanya au tunachofanya. Ni kutokana na kile ambacho Bwana na Mwokozi wetu ameshafanya. Yesu aliharibu mamlaka na nguvu! Neno 'kuharibiwa' lililotumiwa katika tafsiri ya Kiyunani ni apekdýomai, ambayo inamaanisha kupeana silaha, kujinyakua kabisa faida ya mtu binafsi. Aliwapunguza kutokuwa chochote mpaka uwezo wao kututawala
.
Alifanya tamasha la umma la shetani na pepo wake. Hawawezi tena kukutawala kifedha; Nguvu hizi zimepotea! Ni nguvu zillizonyang'anywa mamlaka! Hatujaribu kuwashinda, kubali tu kwa imani yale Yesu aliyofanya. Alichofanya, Alikufanyia! Ushindi wa Kristo ni ushindi wako. Katika familia yako, Kristo tayari ameshinda ushindi. Dai ushindi huo juu ya Shetani katika fedha zako, katika ndoa yako na afya yako.

Haijalishi ni changamoto gani unayokukabili leo. Habari njema ni kwamba Kristo tayari ameshinda ushindi. Adui amepunguzwa kutokuwa kitu, na unaweza kukubali ushindi huo kwako. Anza kutumia mamlaka yako katika Kristo na ufurahie utimilifu wa baraka za Mungu leo.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi si chini ya shetani na majeshi yake. Nimejificha ndani ya Kristo na nimeshinda, kwa kuwa Yeye aliye ndani yangu ni mkuu kuliko yeye aliye ulimwenguni.**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 4:4



**1 Yohana 5:4-5**
**Kwa maana kila aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu. Huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, yaani, hiyo imani yetu. Ni nani yule aushindaye ulimwengu? Ni yule tu aaminiye kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu**

Mwanamume au mwanamke anayemwamini Yesu Kristo ni mshindi. Na tena, alizaliwa kushinda. Katika andiko la hapo juu, tunaelewa kuwa mtu yeyote aliyezaliwa na Mungu tayari ameushinda ulimwengu. Yeye ana chachu ya kuinuka. Haijalishi ni nini kinachomtokea, bado atatoka mshindi. Uliumbwa kutawala; uliumbwa kwa ukuu na utukufu. Umeshinda ulimwengu!
Mungu alijua changamoto zitakazokuja katika ulimwengu huu, na akaunda mtu awezae kuibuka juu ya changamoto zote. Mtu huyo ni kiumbe kipya. Yesu Kristo amekupa maisha ya ushindi. Kataa chochote pungufu.
Neno la Mungu linasema wewe ni zaidi ya mshindi, umezaliwa na Mungu na kushinda kupo kwenye DNA yako. Nenda nje na ushinde kwa jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Nimeundwa kushinda. Sishindani; Natawala kwa jina la Yesu. Nimeshinda ulimwengu; imani yangu ndio ushindi, na ninashinda kila siku.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8:37



**Waefeso 3:19**
**na kujua upendo huu kwamba unapita fahamu, ili mpate kujazwa na kufikia kipimo cha ukamilifu wote wa Mungu.**

Sasa, kujazwa na Mungu ni kujazwa na kila kitu Mungu alicho kwako na alichonacho kwa ajili yako. Kujazwa na Mungu ni kuja mahali pa uzima, afya, amani, utele, na ustawi kamili.Mungu alipokuumba, Alikusudia ukimbie kwa kiwango bora, kama unapojazwa aina sahii ya petroli au mafuta ya taa
.
Utakapogundua jinsi Mungu anavyokupenda sana na ukajilisha juu ya upendo wake kwako, utajazwa kimiujiza ukamilifu wa Mungu. Biblia inatuambia kuwa Mungu mwenyewe ni upendo, na unapojua upendo Wake kwako, unaanza kutembea katika hali ya ki-Mungu ya Mungu. Ndugu na dada, unapoanza kutembea katika upendo, utapata baraka kubwa za Mungu zikilipuka katika maisha yako. Utakuwa sumaku ya baraka

## UKIRI WA KINABII

**Upendo wa Mungu umemwagwa nje moyoni mwangu na Roho Mtakatifu. Ninakataa kutembea kwa hofu na lawama. Nimekubaliwa katika wapendwa. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 4:8, 16



**Waefeso 1:19**
**na uweza wake mkuu usiolinganishwa kwa ajili yetu sisi tuaminio. Uweza huo unaofanya kazi ndani yetu, ni sawa na ile nguvu kuu mno.**

Ndugu na dada, kuna nguvu ndani yako. Iwe unaweza kuisikia au la, bado iko! Shida ya mwamini sio ukosefu wa nguvu! Una nguvu zaidi kuliko shetani yeyote ambaye ametembea uso wa dunia hii. Kama ungejua tu jinsi ya kuingia katika nguvu hii ndani yako.

Paulo anasema, "ukuu mwingi wa dunamis kwa ajili yetu sisi tuaminio," anasema, "kulingana na kazi ya." Vitu vingine hufanya kazi kulingana na kitu kingine. Hiyo inamaanisha kuwa jambo hilo halitafanya kazi bila kitu kingine. Zote mbili ni za kutegemeana. Hivyo anasema, dunamis ubebayo, ni kulingana na kufanya kazi kwa, au energes kwa Kiyunani, kuwezeshwa kwa nguvu Yake kuu.

Unapoanza kuomba katika Roho, hiyo nguvu ya dunamis huchochewa ndani yako. Ndio maana Biblia inasema ya kwamba yeye aombaye kwa lugha isiyojulikana hukua mwenyewe, hupata nguvu mwenyewe. Unapoomba katika Roho Mtakatifu leo, angalia uponyaji huo katika mwili wako, angalia kukua kwako. Hauwezi kusimamishwa kwa jina la Yesu!

## UKIRI WA KINABII

**Uwezo wa Mungu uko ndani yangu, na ninapoomba leo, kila punje ya ugonjwa ndani ya mwili wangu unapotea kwa jina la Yesu! Hofu na unyong'ofu haupo tena, kwa jina kuu la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Yohana 2:27



GoodNews DAILY



**Yohana 14:13-14**
**Nanyi mkiomba lo lote kwa Jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba apate kutukuzwa katika Mwana. Kama mkiniomba lo lote kwa Jina langu nitalifanya.**

Kujuta ya zamani na kuwa na wasiwasi juu ya siku zijazo haitabadilisha chochote. Badala yake muangalie Baba yako wa mbinguni kwakuwa yupo kwa ajili yako wakati huu wa sasa. Unaweza kuwa na uhakika kuwa Yeye atakusaidia na kukutunza.

Mungu alimtuma Mwanae afe kwa ajili yako. Na Yesu alikupa haki ya kununuliwa na damu upate maisha tele yaliyojazwa maana na kusudi! Alikununulia haki ya kutembea katika afya ya kimungu siku zote za maisha yako! Alikupa haki ya utoaji Wake hata uchumi unaposhuka!

Hii ndio sababu aliwaambia wanafunzi wake, "Mnaweza kuomba chochote kwa jina langu, na mtapewa." Una nguvu ya wakili ya kutumia jina hilo la ajabu, na chochote unachokabili leo hakitakuwa na chaguo ila kuinama kwa faida yako.

## UKIRI WA KINABII

**Kwa jina la Yesu, nachukua mamlaka ya fedha zangu. Mungu wangu atatoa mahitaji yangu yote kulingana na utajiri wake katika utukufu.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8:31



**Wagalatia 5:6**
**Kwa maana ndani ya Kristo, kutahiriwa au kutokutahiriwa hakuleti tofauti, bali lililo muhimu ni imani itendayo kazi kwa njia ya upendo.**

Imani hufanya kazi kwa upendo.Mkristo anaporuhusu ugomvi na uchungu moyoni mwake, imani yake inaweza kusonga milima lakini haitamtukuza Mungu kwa sababu yeye hatembei kwa upendo.
Kulingana na Yakobo 3:16, uchungu na ugomvi huchochea machafuko, maangaiko, ghasia, uasi, na kila aina ya ubaya na mazoea mabaya. Ambavyo,kiuhalisia, huzuia huduma ya kweli ya Roho Mtakatifu.
Warumi 10:17 inasema, "kwa hivyo imani huja kwa kusikia na kusikia kwa Neno la Mungu." Imani ya kubadilisha dunia yako huja katika Neno la Mungu. Lakini uchungu, uovu, ugomvi, na hasira zinaweza kuvuta Neno ambalo linastahili kuimarisha imani yako, na hivyo kuchafua na kulifanya lisifanye kazi kikamilifu.
Fanya uamuzi leo kutotunza uchungu na pia kuwa mwepesi kuwasamehe wale ambao labda wamekukosea. Kataa kuwa na kitu dhidi ya mtu yeyote, na imani yako itakuwa nzuri. Unashinda leo

## UKIRI WA KINABII

**Ninachagua kuachilia kila kosa nililotunza na kutembea kwa upendo. Niko huru na uchungu; Niko huru kupenda kwa jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Waebrania 12:15



**2 Wakorintho 4:18**
**kwa sababu hatuangalii yale yanayoweza kuonekana bali yale yasiyoweza kuonekana. Kwa maana yale yanayoweza kuonekana ni ya kitambo tu, bali yale yasiyoweza kuonekana ni ya milele.**

Katika andiko letu la leo, neno la Kiyunani 'kuangalia' linamaanisha kuzingatia, kuweka alama, au kuchukua ufahamu wa. Hivyo, Andiko linamaanisha kutokujali, kuzingatia au kitia mahanani  changamoto zozote unazoweza kukabili katika vita yako ya imani. Badala yake, tazama kila changamoto kama mkate.
Tazama vizuizi kama njia ya kupandishwa daraja. kwani hakuna liwezalo kufanikiwa kusimama dhidi yako kwa sababu wewe ni zaidi ya mshindi. Isaya 54:17 inasema, "hakuna silaha iliyoandaliwa dhidi yako itafanikiwa." Leo, tazama hali zote ambazo zinaonekana kuwa ngumu kama fursa za ushuhuda wako. Haleluya!

## UKIRI WA KINABII

**Naweza kufanya vitu vyote kupitia Kristo anayenitia nguvu. Hakuna kitu kitakachoweza kushindikana kwangu; Mimi ni zaidi ya mshindi!**

**SOMO LA  ZIADA**
Warumi 8:37



**Marko 6:51-52**
**Akapanda kwenye mashua yao na ule upepo ukakoma! Wakashangaa kabisa. Kwa kuwa walikuwa hawajaelewa kuhusu ile mikate, mioyo yao ilikuwa migumu.**

Wanafunzi walipomwona Bwana akitembea juu ya maji, Biblia inasema walishangazwa kupita kiasi. Wasingeweza kuiamini isipokuwa kwa kuona kwa macho yao. Ungekubali kwamba hii ilikuwa maajabu na moja ya ambavyo walikuwa hawajawahi kuona hapo awali.
Lakini angalia kile kifungu kinachofuata kinasema: "Kwa kuwa walikuwa hawajaelewa kuhusu ile mikate, mioyo yao ilikuwa migumu. " Katika akili ya Mungu, hawakupaswa kushangazwa na kutembea Kwake juu ya maji. Kama tu wangeelewa kwamba muujiza wa mikate ulikuwa mkubwa zaidi, wangejua kwamba ilikuwa jambo rahisi kwa Bwana kutembea juu ya maji. Badala yake, anasema mioyo yao ilikuwa migumu.
Unaona, hii ndio sababu maandiko hututia moyo kutosahau faida zake na kushukuru katika mambo yote, haswa tunapomjulisha Mungu maombi yetu. Unaweza kuhamia kwa hali ya juu zaidi ya kiroho wakati unapokubali kila muujiza ambao Mungu amefanya katika maisha yako.

## UKIRI WA KINABII

**Ninashukuru kwa mambo yote makubwa yaliyofanywa maishani mwangu kupitia Kristo, na napokea viwango vya juu zaidi vya kiroho kuona yale ambayo wengine hawaoni kwa Jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Marko 6:51



**Warumi 4:20**
**Lakini Abrahamu hakusitasita kwa kutokuamini ahadi ya Mungu…**

Biblia inasema kwamba tunapaswa kufuata hatua za imani za baba yetu Abrahamu. Hakuwa na wasiwasi katika imani yake. Nataka ugundue kuwa Biblia inasema, " hakusitasita kwa kutokuamini AHADI YA MUNGU." Hiyo inamaanisha kwamba Abrahamu alikuwa na ahadi ya Mungu kwanza kwa chochote kile alichokuwa akisubiri.

Watu hudai, "Sitoumwa kamwe, gari ni langu, kazi ni yangu, hiki na kile ni changu." Lakini mwishowe, huishia kufadhaika, kutokuona matokeo ambayo walifikiria yangekuwa. Hii ni kwa sababu wanaonyesha matakwa yao badala ya kusimama na Neno la Mungu ambalo huwaahidi chochote wanachotamka.

Matumizi ya neno "ahadi" katika Warumi 4:20 ni kuzungumza tu juu ya uhakikishio wa Mungu, dhamana ya Mungu kwa Abrahamu, au kiapo cha Mungu. Chochote unachokabili leo, shikilia kila ahadi za Mungu, kwa maana ni mwaminifu kukuona.

## UKIRI WA KINABII

**Neno la Mungu lina neno la mwisho maishani mwangu. Sitasitasita kwa kutoamini ahadi za Mungu. Hakuna changamoto yoyote itakayonisonga. Ninaendelea kuwa hodari katika Neno kwa jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Yoshua 1:5-8



**Warumi 4:20**
**Lakini Abrahamu hakusitasita kwa kutokuamini ahadi ya Mungu, bali alitiwa nguvu katika imani yake na kumpa Mungu utukufu**

Waumini wengi, wanapokabiliwa na hali ngumu, wanaonekana kuwa na machaguzi mengine mengi. Lakini wanaposhindwa wote, ghafla hugundua, wacha nijaribu Mungu. Katika andiko letu hapo juu, Abraham hakuiacha imani yake kwa dalili za kuchelewa. Alishikilia sana ahadi Mungu alitoa aliposema Nitakufanya kuwa baba wa mataifa (Mwanzo 17: 4).
Inasema, "hakusitasita." Kwa maneno mengine, alikataa kuangalia hali na uhalisia. Akachimba visigino vyake ardhini na kusema "ni njia ya Mungu au hakuna njia kabisa" mpaka ahadi yake ilipotimizwa. Imani yako iko wapi leo? Je! Imewekwa chini ya mwamba mahali fulani au inazunguka kwenye kabati nyuma ya unga uliomalizika miaka miwili iliyopita?
Leo, weka imani hiyo kazini. Usiitoe! Usikate tamaa! Jikaze na umpe Mungu utukufu kupitia hayo yote. Simama juu ya hilo Neno hilo na uamshe imani yako.

## UKIRI WA KINABII

**Imani yangu inanifanyia kazi. Ni imani dhabiti. Imani yangu inatimiza mambo makubwa, na ninategemea nguvu ya maisha yangu, Yesu Kristo, na kushinda kwa jina la Yesu. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Waebrania 11:6



**1 Wakorintho 13:1-2**
**Hata kama nitasema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa kengele inayolialia au toazi livumalo. 2Ningekuwa na karama ya unabii na kujua siri zote na maarifa yote, hata kama nina imani kiasi cha kuweza kuhamisha milima, kama sina upendo, mimi si kitu.**

Je! Unatambua kuwa zawadi zote za kiroho ni dhihirisho la upendo wa Mungu kwetu hivyo haziwezi kuwa kubwa kuliko upendo?

Hii ndio sababu tunapozaliwa mara ya pili, Upendo wa Mungu umiminwa kutoka kwenye. Mioyo yetu na Roho Mtakatifu. Umejaliwa uwezo wa kutembea katika upendo na kufanya kazi kama Mungu. Inakuwa asili yetu kupenda. Hii ndio sababu Paulo alisema nanaweza kunema na lugha za malaika lakini bila upendo haina maana.

Fanya upendo kuwa matakwa yako makubwa leo. Kabla ya kufanya harakati, jiulize kama upendo ndio nia yako ya kuifanya. Unapoamka kila asubuhi, amua kuonyesha upendo hata kwa wale ambao unadhani hawafai. Huo ni upendo wa kweli. Warumi 5:5 inasema pendo la Mungu limemiminwa katika mioyo yetu  na Roho Mtakatifu tuliyepewa sisi. Kama waumini inamaanisha kuwa kila mmoja wetu ana uwezo wa kupenda visivyopendeka. Fanya UPENDO uwe hamu yako kubwa, anza sasa

## UKIRI WA KINABII

**Napenda kwa sababu baba yangu ni upendo. Dhamira yangu leo ni kufanya upendo takwa langu kubwa. Nachagua kupenda!**

**SOMO LA  ZIADA**
1 Yohana 4:7



**Warumi 1:16**
**Kwa maana siionei haya Injili kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.**

Ile dakika ambayo unasoma ama kusikia habari njema, na unaipokea na kuiamini, neno lake linatenda sozo (neno la kiyunani lenye maana ya kuokoa); linakufanya mkamilifu kwa kila namna, kwasababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu, kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.

Habari njema ni ipi? Ni kwamba Mungu anakupenda sana mpaka akamtoa mwana wake wa pekee kupigwa ili tuweze kupata baraka zake bila kuzifanyia kazi.

Miugiza haitokei kwasababu umefanya taratibu fulani kwa uaminifu, ila ni kwasababu ya kusikia habari njema na kuiamini.

## UKIRI WA KINABII

**Niko vile ambavyo neno la Mungu linasema na ninaweza kufanya kile ambacho neno lake linasema. Nimekamilika na sitokubali chochote pungufu katika jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 2:4



**Zaburi 20:7**
**Wengine wanatumaini magari ya vita na wengine farasi, bali sisi tutalitumainia jina la BWANA, Mungu wetu.**

Ni jambo la kushangaza kujua kuwa kama waumini katika Yesu tunaye rafiki aliye karibu kuliko kaka. Hii ndio sababu alisema, Sitakuacha kamwe, wala kukutelekeza, nitakuwa nawe katika nyakati ya shida. Yeye ndiye mbadilishaji asiyebadilika. Ambaye anakujua kuliko unavyojijua.

Nanga yetu na tumaini linapaswa daima kuwa ndani ya Kristo, tunayo faida juu ya mifumo ya ulimwengu. Ni kitu hatari kujiaminisha na vitu vya ulimwenguni. Unaona, uchumi ukishindwa, Bwana hatoshindwa. Waganga bora kabisa wamaposhindwa kupata tiba, Mungu hatashindwa.

Hata wapendwa wako wanapokuacha, yeye ndiye anayebaki amesimama nawe kama alivyoahidi kwamba hatawaacha kamwe au kuwatekeleza. Hii ni sababu andiko linasema anamweka kwa amani kamilifu ambaye akili yake imekaa juu yake. Acha Mungu awe mtu unayemtegemea leo  hautasikitishwa kamwe.

## UKIRI WA KINABII

**Leo nachagua kuweka tumaini langu kwa Bwana kwani hakika hataniacha wala kunitelekeza. Yeye ndiye chanzo change pekee kwa kila kitu na nimebarikiwa kama matokeo yake!**

**SOMO LA  ZIADA**
Zaburi 46:1



**1 Corinthians 1:26**
**Ndugu zangu, kumbukeni mlivyokuwa mlipoitwa. Kwa kipimo cha kibinadamu, si wengi wenu mliokuwa na hekima. Si wengi mliokuwa na nguvu, si wengi mliozaliwa katika jamaa zenye vyeo.**

Unaposoma hivi sasa unaweza kudhani kuwa wewe si kitu, ambaye amekuwa au mkosaji machoni pa ulimwengu. Nina habari njema kwako, Nena la Mungu linasema kwamba ikiwa hauna hekima, hauna nguvu au si mtukufu kulingana na mwili, basi wewe ni mgombea mkuu wa Yeye kukuita!

Utaalam wake ni kutumia wasio na vikwazo. Wale ambao hawajui ili awafanye wajue. Atakapoanza kukutumia, utaona neema Yake, nguvu na ongezeko yakibadili maisha yako. unapofikiri kuwa wewe ni dhaifu na mdogo ikilinganishwa na wengine ulimwenguni, hapo ndipo Mungu anaweza kukutumia kufanya makubwa na vitu vya ajabu kwake!

Nguvu yake imefanywa kamili katika udhaifu na unakaribia kugeuza meza juu ya adui ambaye alifikiri amekuweka chini usiwe kitu.

## UKIRI WA KINABII

**Kupanda daraja ni kwangu leo sio kwa sababu mimi nina vifaa kamili lakini kwa sababu Mungu ameniandaa. Nguvu yake inafanywa kamili katika udhaifu wangu kwa jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
2 Wakorintho 12:9



**Wafilipi 4:19**
**Naye Mungu wangu atawajaza ninyi kila mnachohitaji kwa kadiri ya utajiri wake katika utukufu ndani ya Kristo Yesu.**

Mara nyingi nimesikia watu wakisali aya hiyo hapo juu bila maarifa kamili au ufunuo. Tunahitaji kuelewa hili Andiko kutoka kwa mtazamo wa mwandishi. Chukua muda kuona kile kilichomsababisha mwandishi kuandika alichoandika.

Kwanza, hii ilikuwa barua kutoka kwa mtume Paulo kwenda Kanisa lililoko Filipi. Kanisa lilielewa jukumu lao la kusaidia huduma kwa uhakika kiasi kwamba Mtume Paulo ilibidi atangaze hiyo kwa sababu ya ushirika, Mungu wa Mtume Paulo atawajaza na kukidhi mahitaji yote ya wale walioshiriki. Unaona hiyo?

Unapokuwa mfadhili wa ufalme, hauwezi tena kukabiliwa na ukosefu wowote katika eneo lolote la maisha yako, iwe fedha, afya au mahusiano. Kwa kuwa Mungu amesha andaa nguvu Zake za kukukidhi kutakao dumu kwako.Na juu ya hiyo, Neema yake na zaidi ya neema yake! Kama nabii wa Mungu, ninaamua na kutangaza kila hitaji katika maisha yako likutwe kwa jina la Yesu. Kuna wingi wa kutosha katika Kristo. Upokee sasa.

## UKIRI WA KINABII

**Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa kitu chochote kizuri. Mimi hupewa kutoka juu, kwa maana namtumikia Mungu wa zaidi ya kutosha.**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 6:9



**Yohana 14:26**
**Lakini huyo Msaidizi, yaani, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atamtuma kwenu kwa Jina langu, atawafundisha mambo yote na kuwakumbusha yote niliyowaambia.**

Kama mwamini mpya wa uumbaji, unapaswa kufanya kazi kutoka mwelekeo tofauti na wajuao ulimwengu.Umeitwa kuonyesha hekima na utukufu wa Mungu. Uliumbwa kufanya kazi na hekima ya aina ya tofauti. Haupaswi kamwe kung'aa gizani bila suluhisho la maswala ya maisha.

Biblia inasema Roho Mtakatifu atakufundisha vitu vyote. Ndio, kukufundisha mambo yote! Je! Unaamini hivyo? Au wewe ni kama wale wanaoamini unatafuta ushauri wa Mungu kwa vitu vya kiroho tu lakini julisha wasaidizi wa "kitaalam" kwa vitu vingine vyote maishani mwako?

Yeye ndiye Mbunifu wa ajabu wakati biashara yako inaugua, na ndoa yako ikiwa kwenye miamba. Unapoenda nje leo, unabeba huu msukumo wa Roho Mtakatifu, na hakuna kitu kama yasiyowezekana kwako. Una shauri kubwa kuliko yote katika Yesu.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi sipo bila msaada. Mwana mkakati wa ajabu yuko upande wangu. Nimepokea msukumo kufanya kazi na kushinda kila wakati.**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 16:13



**Mathayo 8:8**
**Lakini yule jemadari akamwambia, "Bwana, mimi sistahili wewe uingie chini ya dari yangu. Lakini sema neno tu, naye mtumishi wangu atapona.**

Mkuu huyo hakuwa hata Myahudi, lakini alielewa imani kiasi kwamba Yesu alisema alikuwa hajaona imani kubwa sana ya hivyo Israeli yote. Imani ya mkuu wa jeshi ilionekana katika kuamini kwake kuwa neno lolote linalosemwa na Mwalimu lingeweza kutosha kumponya mtumwa wake. Aliamini neno la Yesu na amri ya mamlaka juu ya magonjwa.

Unaona, ofisa wa jeshi alielewa vyeo vya jeshi.Alielewa Yesu kuwa Mwana wa Mungu, hivyo mamlaka yake kuwa makubwa kuliko ugonjwa wowote. Alichohitaji na kutaka ilikuwa neno lisemalo mtumwa wake amepona.

Mamlaka inasema unajua wewe ni nani na una nguvu ya kuamuru na kutangaza jambo na liwe. Hiyo mamlaka inakupa nguvu za kuongea kwa hali katika maisha yako zitoweke, au ugonjwa au huyo pepo ya unyogovu au upweke uache kukukandamiza. Leo upako huo wa mamlaka uko tayari kwa kila mwamini, lakini unahitaji tu kuamini na kutenda juu yake kwa kufungua mdomo wako na kuongea.

## UKIRI WA KINABII

**Kristo ndani yangu ndio mamlaka yote ninayohitaji. Natembea kikamilifu katika mamlaka haya juu ya magonjwa, kifo na ukosefu. Ninaamini, na hivyo natamka leo kwa Jina la Yesu**

**SOMO LA ZIADA**
Yohana 6:9



**Waebrania 4:12**
**Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo.**

Kwenye andiko letu hapo juu, neno limefananishwa na kitu kikali ambacho ni upanga. Neno la kiyunani la mdomo ni "stoma" , linalomaanisha kukata, maneno hasi yaliyonenwa juu yetu yanaweza kukata hatima zetu. Hii ndiyo sababu maneno yako yanatakiwa kujazwa na matumaini pamoja na imani.

Neno ni silaha yako ya kubomoa, kufuta na kukata kila hali hasi na maneno mabaya. Unaweza kuamini ndani ya moyo wako vyovyote upendavyo lakini kama mdomo wako ukikaa kimya, hakuna kitakachobadilika. Biblia inasema kwamba mauti na uzima huwa katika uwezo wa ulimi na wak waupendao watakula matunda yake.

Neno ni jambo lenye nguvu zaidi ulimwenguni. Isitoshe, dunia zimebwa kwa maneno yaliyotamkwa. Neno limeumba dunia. Imani haitokwenda kuzidi ukiri wako. Anza kunena ukiri wako na ruhusu ukutengenezee njia. Panda juu unavyonena na kuachilia nguvu ya neno juu ya hali zako. Nakuona ukipanda juu.

## UKIRI WA KINABII

**Mungu anataka kujionesha kupitia mimi. Haijalishi ni lipi limesemwa kinyume nami. Hivi leo, ninakata kila neno hasi na la mashaka linalotaka kuharibu hatima yangu. Ninatamka uhai leo na ninavuna matunda.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 10:9



**Mwanzo 37:28**
**Wakapita wafanya biashara Wamidiani basi wakamtoa Yusufu, wakampandisha kumtoa katika birika, wakamwuza Yusufu kwa Waishmaeli kwa vipande vya fedha ishirini nao wakamchukua Yusufu mpaka Misri.**

Je, unaweza kupata picha kilichokuwa kinaendelea kwenye akili ya Yusufu alipokuwa ndani ya shimo? Ndugu zake walimuuza kwa vipande ishirini vya fedha. Walimbeza kwa kumuita bwana wa ndoto, wakamvua kanzu yake ya rangi nyingi na kumtupa kwenye birika wakidhani amekufa.

Ilikuwa kama maisha yake yalifika mwisho, ila Mungu alibadilisha mambo na Yusufu akajikuta kwenye jumba la Mfalme tajiri kuliko wote duniani kwa wakati ule. Kaka zake walipoomba msamaha kwa kumuuza, aliwaambia:
Mwanzo 45:5 " Basi sasa, msihuzunike, wala msiudhike nafsi zenu, kwa kuniuza huku maana Mungu alinipeleka mbele yenu kuhifadhi maisha ya watu."

Ndiyo maana mtume Paulo alikuwa na ujasiri wa kusema, " MAMBO YOTE HUFANYA KAZI KATIKA KUPATIA MEMA." Hakusema mambo baadhi, ila mambo yote na inajumuisha milango iliyofunguliwa na kufungwa.

## UKIRI WA KINABII

**Mambo yote hutenda kazi kunipatia wema. Makosa yangu yote ni kwaajili ya mimi kuanguka mbele, na japo kuwa naweza anguka mara saba, nitanyanyuka na kubaki nikisimama. Kwavila nampenda Mungu na nmeitwa kwa kusidi lake. Nakushukuru, Baba, kwa milango iliyofungwa katika jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Warumi 8:28



**Yakobo 3:5-6, 8**
**Vivyo hivyo ulimi nao ni kiungo kidogo, nao hujivuna majivuno makuu. Angalieni jinsi moto mdogo uwashavyo msitu mkubwa sana. Nao ulimi ni moto ule ulimwengu wa uovu, ule ulimi, umewekwa katika viungo vyetu, nao ndio uutiao mwili wote unajisi, huuwasha moto mfulizo wa maumbile, nao huwashwa moto na jehanum. Bali ulimi hakuna awezaye kuufuga ni uovu usiotulia, umejaa sumu iletayo mauti.**

Maneno unayozungumza yatakuweka juu ama chini maishani. Unaona, unaweza kunena na kutoka kwenye matatizo.

Tazama ambavyo ulimi una nguvu. Neno la Mungu ambalo limetungwa moyoni mwako, halafu likaundwa na ulimi wako na kutamkwa na mdogo wako, linakuwa nguvu ya kiroho inayoachilia uweza wa Mungu ndani yako. Mdomo wako sio wa kula tuu. Unafanya kazi kuu ya kuumba upya ulimwengu wako. Zungumza na utoke kwenye matatizo na uone ulimwengu wako ukiumbika upya!

## UKIRI WA KINABII

**Katika jina la Yesu, ninaumba upya ulimwengu wangu. Pale kwenye matatizo, natamka urejesho. Ambapo adui ameweka gharika, marumbano, na upepo, natumia mdomo wangu kutamka “amani.” Katika jina la Yesu, ulimwengu wangu unabadilika ninavyochora njia ya maisha yangu kwa mdomo wangu.**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 18:21



**Wafilipi 4:13**
**Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu.**

Nimesikia watu wengi ambao kipindi wakiwa wanakuwa, waliambiwa maneno mengi kama vile, "hautokuwa lolote. Hautofanikiwa. Wewe ni wa kufeli. Hauwezi kufanya jambo hili ama lile, familia yetu haiwezi kuvuka mpaka fulani." Ninayo HABARI NJEMA kwako. Umejaa sana kushindwa. Wewe ni mvunja mipaka, ukingo. Ambavyo familia yako ilishindwa kufanya, wewe utafanikisha. Anga sio kikomo chako. Hauna kikomo!

Tazama, unao ukuu ndani yako kwenye mfumo wa Yesu Kristo. Wewe sio Suzani ama Yohana wa kawaida. Wewe ni mtengneza hatua na mnyanyua viwango kwenye familia yako. Wanakutazamia wewe kwasababu kwako, kufeli hakuwezekani daima.

Leo, tembea kwenye kweli inayokutambulisha ndani ya Kristo. Wewe ni mshindi, uliyeumbwa kufanikiwa na kustawi. Kushindwa haiko ndani ya DNA yako.

## UKIRI WA KINABII

**Mimi ni mshindi. Ninastawi. Sishindwi, siwezi kushindwa. Mimi ni mvunja mipaka. Mimi ni mvuka mipaka. Ninayaweza yote kupitia Kristo katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
Zaburi 1



**Wakolosai 3:16 Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu.**

Neno la Mungu likizidi ndani yako, litashinda. Andiko tunalofungulia leo linatusihi kuruhusu neno la Kristo likae kwa wingi ndani yetu.

Mungu hataki ukose lishe bora inapokuja kwenye swala la neno la Mungu. Anataka neno la Mungu kuishi mdani yako kwa wingi. BWANA YESU alisema, "kinywa cha mtu hunena yale yaujazayo moyo wake." Huwezi kunena ambayo hujasikia. Hivyo cha kwanza ni kuchukuwa muda kusoma, kusikia na kutafakari neno. Neno litabadili vile ambavyo unawaza. Ghafla utaanza kunena, "siwezi kushindwa. Siwezi kuugua. Nimeyashindamagonjwa. Nimeshinda mauti. Nilifufuliwa pamoja na Kristo." Neno litachukuwa uskani kwenye mwili wako na magonjwa yatashindwa.

## UKIRI WA KINABII

**Neno la Mungu linakaa ndani yangu kwa wingi. Mimi niko vile ambavyo neno la Mungu linasema, na ninaweza kufanya yale ambayo neno linasema ninaweza kufanya. Neno ndani yangu linazaa matunda katika jina la Yesu.**

**SOMO LA ZIADA**
Matendo ya Mitume 20:32



**Waefeso 3:20**
**Basi atukuzwe yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu**

Je, unafahamu nguvu uliyonayo ndani yako? Hakika Mungu tunaemtumikia ni mwenye nguvu yote; na ndani yake vyote vinawezekana. Ni muhimu kufahamu kweli hii, nguvu ya kuleta mabadiliko. Nguvu yake ya kusababisha muujiza unaotamani iko ndani yako tayari! Ni jukumu lako kuiamsha.

Kama tunavyoona kwenye maandiko hapo juu, tunajifunza kwamba chochote ambacho Mungu atafanya kwenye maisha yako kitalingana na nguvu ifanyayo kazi ndani yako.

Siku ya leo, amsha nguvu ya Mungu ndani yako kwa kukiri neno lake kwa ujasiri. Mungu na neno lake ni kitu kimoja. Unapokiri neno lake kwenye hali yeyote, unasababisha nguvu yake kuleta mabadiliko kwenye hali hiyo. Kama unataka kuona nguvu ya Mungu ikiachiliwa kwenye maisha yako, dumisha tabia ya kutafakari neno lake, fikiria na nena neno.

## UKIRI WA KINABII

**Leo ninaamsha nguvu ya Mungu ifanyayo kazi ndani yangu ili kuleta mabadiliko kwenye hali zangu kwa kukiri, kunena na kutafakari neno lake. Maisha yangu yatazaa matunda katika jina la Yesu**

**SOMO LA ZIADA**
Mathayo 17:20



**1 Wakorintho 14:4**
**Yeye anenaye kwa lugha hujijenga nafsi yake bali ahutubuye hulijenga kanisa.**

Watu wengi hushanjaa juu ya hatua za kunena kwa lugha. Wengine wanaenda mbali mpaka kuuliza kama ni sawa kuiga lugha, na wengine wanauliza kama ni sahihi kuimba na kuongea kwa lugha. Jib uni sahihi, lipo kwenye mstari hapo juu.

Mstari wetu wa leo unaonesha kwamba yule anenae kwa lugha hujojenga nafsi yake kwenye na kuamsha nguvu ya kiungu ndani yake. Neno la kiyunani lililotumika kutafsiri "hujijenga" ni neno oikodoméō, lenye maana ya kujenga ama kusimamisha jengo. Hivyo, unapozungumza kwa lugha, hauzungumzi maneno yasiyo na maana, lakini unajijenga kuepukana na magonjwa. Yule anenae kwa lugha anajiongezea nguvu kama kuchomeka betrii kwenye umeme. Mtu huyu hatoishiwa nguvu wala kufa  kwasababu atakuwa na mfumo wa kujijenga mwenyewe ndani ya roho yake.

## UKIRI WA KINABII

**Nachagua hivi leo kunena mfululizo kwa lugha, ninajiongezea nguvu mwenyewe kama betrii; ninajijenga. Ninaamsha nguvu iliyoko ndani yangu.**

**SOMO LA  ZIADA**
1 Wakorintho 14:18



**Zaburi 103:20**
**Mhimidini Bwana, enyi malaika zake, Ninyi mlio hodari, mtendao neno lake, Mkiisikiliza sauti ya neno lake.**

Kuna jambo sitaki ukose kwenye andiko letu la leo. Maandiko yanasema malaika "wasikiliza sauti ya neno lake." Sasa ni nani anaelipa neno la Mungu sauti? Ni wewe! Kila mara unapotamka neno la Mungu, unalipa sauti neno lake. Pale malaika wanaposikia sauti ya neno lake, wanalitendea kazi!

Hivyo, wanapokusikia unasema, "asante Baba, hakuna jambo baya litakalonikumba wala pigo lolote kusogelea maskani yangu" watakuja kukusaidia kwa maana wanasikia ukilipa sauti neno la Mungu. Hata kama hauna uwezo wa kuusema mstari kwa usahihi, watakuja kukuokoa.

Jambo lolote unalopitia leo, lipe sauti neno la Mungu na ukaone malaika wakichukuwa hatua. Malaika wake wanaingia kazini kwaajili yako pale ambapo unalitamka neno la Mungu.

## UKIRI WA KINABII

**Mafanikio ni urithi wangu katika jina la Yesu. Malaika wako kazini ili kunipandisha cheo. Haleluya!**

**SOMO LA ZIADA**
Waebrania 4:14



**1 Yohana 5:4**
**Kwa maana kila kitu kilichozaliwa na Mungu huushinda ulimwengu na huku ndiko kushinda kuushindako ulimwengu, hiyo imani yetu.**

Andiko letu la hapo juu linafurahisha sana. Mtume Yohana hataki tukose jambo muhimu sana hapa. Anasema kwamba hatujaribu kuushinda ulimwengu, tumekwisha kufanya hivyo kwa kweli ya kwamba tumezaliwa na Mungu.

Kuzaliwa na Mungu inamaana Baba yet uni Mungu. Hii inamaana kwamba tumebeba mbegu yake, na tumebeba DNA yake. Hivyo basi, tumekwisha mshinda ibilisi na majeshi yake. Amka kwenye kweli hii na usimamie ushindi wako kwa kunena maneno yaliojaa imani.

## UKIRI WA KINABII

**Ninakiri kwamba natembea kwenye ushindi na ninakuwa kwenye imani kutoka utukufu hadi utukufu. Mimi ni zaidi ya mshindi kwenye maisha haya katika jina la Yesu!**

**SOMO LA ZIADA**
1 Petro 1:23



**Mithali 22:6-7**
**Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee. Tajiri humtawala maskini, Naye akopaye ni mtumwa wake akopeshaye.**

Hili ni andiko ambalo linawachanganya wengi lakini ukilitazama kwa umakini, kila kitu kipo hapo kwenye maandiko. Tumekuja na mafundisho ya kila aina kutoka kwenye andiko hili wakati majibu yapo kwenye mstari unaofuata.


Tajiri humtawala maskini, naye akopaye ni mtumwa wa akopeshaye. Ndivyo hivyo! Hicho ndicho tunatakiwa kuwalea watoto wetu. Kuwaeleza ya kwamba wanatakiwa kuwa watoaji na sio wapokeaji. Wao ni kichwa na sio mkia. Tazama, mwanamume kwenye haki huacha urithi kwaajili ya watoto na wajukuu wake.

Haya ndiyo mambo tunatakiwa kufundisha vizazi vijavyo. Tumeitwa kuwezesha kizazi kijacho na kuacha urithi wa kimungu kwaajili yao. Jinsi tuwaleavyo watoto wet uni juu yetu, lakini biblia inatuonesha ni mambo gani ya kutia mkazo.

## UKIRI WA KINABII

**Watoto wangu hawatokosa ama kukumbwa na njaa navyowafunza kila mara njia za Mungu. Wametiwa nguvu kufanikiwa na hawatoondoka kwenye urithi wao.**

**SOMO LA ZIADA**
Mithali 4:5




GET YOUR COPY NOW!

BEBE ANGEL

# GRACE DRIVEN LIFE

PROVEN STEPS TO LIVING A GUILT FREE LIFE

www.uebertangel.org | www.bebeangel.org

SPIRIT EMBASSY

TheGoodNewsChurch®

WITH **UEBERT & BEVERLY 'BeBe' ANGEL**


TheGoodNewsWorld Helplines
USA: +1 (240) 781-6942
UK: +44 333 344 8612
RSA: +27 (51) 004-0209
www.goodnewsworld.com